

Biashara

Vanilla iliyoahidi
utajiri yawaangamiza
wakulima Kagera

Habari Uk. 22



Rushwa

Vuta nikuvute
Takukuru vs
Dkt Mollel

Habari Uk. 16



Siasa

Kilichofanya
Dkt Tulia
kujitosa
Uyole

Habari Uk. 20



CCM yaanika jeuri



Kwanza ni kuongezeka kwa
ukuaji wa uchumi kutoka
asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi
asilimia 5.5 mwaka 2024,
kuongezeka kwa wastani wa
pato la mtu mmoja mmoja
kutoka shilingi 2,468,241
mwaka 2020 hadi shilingi
3,204,244 mwaka 2024...”
Prof Kitila Mkumbo

Habari Uk. 6&7

Rais Samia
Suluhu
Hassan
kulia,
akiwa na
Katibu Mkuu
CCM, Dkt
Emmanuel
Nchimbi



...Mkakati wake kuvuta kura

Uk. 14

Tahariri/Katuni

Tume ya Maadili iongezewe wajumbe

TUME ya Maadili ni moja ya vyombo muhimu nchini. Tume hiyo, ambayo ipo chini ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ina wajibu wa kusikiliza mashauri yote yanahusiana na viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya uongozi kati ka sehemu zao za kazi.

Tume hii, ambayo inaundwa na wajumbe watatu – wote wakiwa ni majaji – inafanya kazi zake kwa mtindo wa mahakama.

Husikiliza mashauri yote ya viongozi wa umma wanaotuhumiwa kwa ukiukwaji wa maadili. Lakini ukiangalia akidi yake – watu watatu – unapata wasiwasi na mashaka iwapo

Tume hiyo kweli inafanya kazi zake kwa ufanisi.

Wimbi la malalamiko ya wananchi linaonyesha kuwa tatizo la maadili miogoni mwa viongozi ni kubwa.

Inapotokea mmoja wa wajumbe akawa na udhuru, inakuwa vigumu kwa Tume hiyo kufanya shughuli zake kwani wajumbe wawili watakuwa hawajatimiza akidi inayotakiwa kwa Tume hiyo kutoa uamuzi ambao utasimama kisheria.

Sisi wa Pambazuko tunaona akidi hiyo ya wajumbe wa Tume ya Maadili kuwa ni kikwazo kwa Tume hiyo muhimu kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Tunashauri kuwa idadi ya wajumbe wa Tume hiyo iongozwe ili kuipa Tume wigo mpana zaidi wa watendaji ndani yake.

Idadi kubwa ya wajumbe itaiwezesha Tume kufanya vikao vingi kuendesha mashauri kuhusiana na viongozi wanaotuhumiwa kukiuka maadili.

Kama Tume ikiwa na wajumbe wengi inaweza hata kufanya vikao zaidi ya kimoja kwa wakati mmoja, huku wajumbe wakijigawa katika makundi.

Lakini pia idadi kubwa ya wajumbe itatoa wigo mpana zaidi wa masuala yanayofikishwa mbele ya Tume kujadiliwa kwa upana kwani wahusiika watakuwa wengi zaidi na hivyo kupata mawazo mengi zaidi katika kujadili masuala mbalimbali yanayofikishwa mbele ya Tume.

Wananchi wakiona mashauri mengi zaidi ya maadili dhidi ya viongozi wao yanasikilizwa na kutolewa uamuzi, nao watapata mwamko wa kuripoti matukio mengi zaidi ya ukiukwaji wa maadili yanayofanywa na viongozi wao.

Katuni



Wanafunzi bungeni...



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Anlex ya Jijini Dar es Salaam, wakifuatilia kikao cha Bunge la 12 wakati wa ziara ya kimasomo waliyoifanya bungeni Dodoma mwishoni mwa wiki. (Picha na Mpigapicha Wetu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Habari katika picha

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Songwe, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP), Charles Bukombe akikagua basi la abiria wakati wa ukaguzi wa magari ya abiria na mizigo katika kituo cha ukaguzi wa magari eneo la Chimbuya Wilaya ya Mbozi mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Watu)



Mke wa Hayati Rais Dk. John Magufuli, Janet Magufuli akifurahia jambo na Mariam Mwinyi (kulia) ambaye ni mke wa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi walipo-hudhuria Mkutano Mkuu Maalum Dodoma mwishoni mwa wiki.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, akimpima kipimo cha kuangalia kilevi dereva wa lori wakati wa ukaguzi wa magari ya abiria na mizigo katika kituo cha ukaguzi wa magari eneo la Chimbuya Wilaya ya Mbozi mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Watu)



Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waki-onyesha mabango ya mikoa wanayoto-ka wakati wa mku-tano mkuu malaam juzi.

Dunia: Hapa na Pale

Majambazi yaiba divai

HAKIKA dunia haiishi vituko. Majambazi waliovunja kanisa na kuiba vifaa, pia walikula sakramenti na kunywa divai kabla ya kutoweka.

Tukio hilo lilitokea wiki iliyopita katika Kanisa la Anglikana la Mtakatifu Mathayo Mutithi kwenye Kaunti ya Kirinyaga, Kenya. Waliiba vifaa vyenye thamani ya Shilingi 120,000 usiku wa Jumapili iliyopita, Mei 25, 2025.

Inaelezwa kuwa majambazi hao walivunja madirisha na kufanikiwa kuingia ndani ya kanisa hilo wakiwa na lengo la kuiba sadaka zilizokusanywa Ibada ya Jumapili.

Viongozi wa kanisa hilo na baadhi ya waumini wenye kawaida ya kusali kila asubuhi, walishangwa kutoona baadhi ya vifaa ndani ya kanisa na kugundua kutokea kwa wizi huo. Vifaa vingi vya muziki na sauti na vyombo kadhaa vya kutolea huduma kwa waumini pia vilitoweka.

Marufuku kuuza mapanga

SERIKALI ya Jimbo la Victoria nchini Australia, imepiga marufuku kuuzwa kwa mapanga kiholela.

Sasa inatazamia kupitisha sheria kali zaidi kwa maduka kuuza mapanga, kwani yamekuwa yakitumika kujeruhi watu, hasa wanaokuwa kwenye ugomvi.

Waziri Mkuu wa jimbo hilo, Jacinta Allan Jumatatu iliyopita, alitangaza kuwa marufuku hii itaanza kutekelezwa hivi karibuni baada mapigano yaliyohusisha matumizi ya mapanga katika eneo moja la biashara la Melbourne



Avocado yakamiwa kodi

SASA huenda zao la avocado linalosafirishwa kutoka Kenya kwenda nje ya nchi hiyo likaanza kutozwa ushuru. Zao hilo halikuwahi kuwa na kodi ya aina yoyote kabla.

Ushauri huo umeelekezwa na Benki ya Dunia kwa Kenya huku ikishauri kuwekwa kwa Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) ya asilimia 16 kwa bidhaa zingine za msingi kama nyama, unga wa ngano na kahawa.


Benki hiyo ya dunia inaeleza kuwa avocado ni zao lenye kubeba ishara za anasa na kwamba kuwekwa kwa ushuru huo kutaifanya Kenya kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 78.4 zaidi.

Putin sasa akera Trump

RAIS wa Marekani, Donald Trump ameelezea kukerwa na swahiba wake, kiongozi wa Urusi, Vladimir Putin.

Ameeleza wazi kukerwa huko baada Urusi kufanya mashambulio mabaya zaidi nchini Ukraine wiki iliyopita. Mashambulizi hayo yaliua idadi kubwa ya watoto.

Huku akimkaripia vikali Putin, na kumuita kuwa ni mwendawazimu kupindukia, Trump



Rais wa Urusi,
Vladimir Putin

alisema; “Sijui kimempata nini tena, anaua watu wengi zaidi sasa. Haiwezekani hali ikaendelea hivi na sisi kukaa kimya tu, lazima tukemee?”

Habari Kuu

CCM yaanika jeuri



Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, akifurahia jambo wakati mkutano mkuu wa chama hicho, Dodoma juzi.

Na Waandishi WETU, Dodoma

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetangaza mafanikio kiliyofikisha kwa Watanzania kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Katika taarifa yake kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum na Watanzania, Ijumaa iliyopita – Mei 30, 2025 – jijini Dodoma, chama hicho tawala kilieleza kujivunia maendeleo kwa Tanzania, huku kikionyesha jeuri ya utekelezaji wake.

Mafanikio hayo ya utekelezaji wa CCM, yanayoweza kuelezwa kuwa ni “jeuri ya utekelezaji” yalibainishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo.

“Kipindi cha awamu ya sita, kilikumbwa na misukosuko mbalimbali ikiwemo janga la UVIKO-19, pamoja na migogoro ya kimataifa ambayo iliathiri uchumi wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania...”

“Pamoja na hali hiyo, serikali ilitekeleza mikakati mbalimbali ya kisera, kiutawala na uwekezaji katika miundombinu ya sekta za usafirishaji, nishati, elimu, maji na afya ili kukabiliana na changamoto hizo na mikakati hiyo imewezeshwa kupata mafanikio yafuatayo...”

“Kwanza ni kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.5 mwaka 2024, kuongezeka kwa wastani wa pato la mtu mmoja kutoka shilingi 2,468,241 mwaka 2020 hadi shilingi 3,204,244 mwaka 2024...”

“Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani kutoka shilingi trilioni 20.59 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 28.83 mwaka 2023/2024...”

“Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2024/2025, kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya shilingi trilioni 25.67 zimekusanywa...”

“Vilevile, katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Machi, 2025, jumla ya shilingi trilioni 120.16 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani na kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 103.87 ni mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania...”

“Aidha, mapato ya ndani yaliyokusanywa kwa mwezi yameongezeka kutoka shilingi trilioni 1.51 Novemba, 2020 hadi shilingi trilioni 3.09 Machi, 2025 na mapato hayo yameiwezesha serikali kuendelea kuboresha hali ya maisha ya wananchi kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii zikiwamo afya, elimu na maji...”

“Pia uimarishaji wa miundombinu wezeshi ya uwekezaji na biashara ikiwamo nishati na uchukuzi,” alisema Profesa Kitila na kuongeza.

“Vilevile, mfumuko wa bei umeendelea kuwa himilivu na kubaki ndani ya lengo la nchi ambalo ni chini ya asilimia tano na Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika...”

“Wastani huo wa mfumuko wa bei umeendelea kulinda pato la mwananchi mmoja mmoja na kumwezesha kununua bidhaa zaidi na hivyo kuchangia kuboresha maisha na kwa upande wa wawekezaji na wazalishaji, hali hiyo imeondoa wasiwasi wa mabadiliko ya bei na hivyo kuchangia kuongeza uwekezaji...”

Inaendelea Uk. 7

Habari Kuu



Mwenzekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar (kushoto) na Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi, wakionyesha ilani ya uchaguzi ya mwaka 2025/2030 baada ya kuzinduliwa, Dodoma juzi.

CCM yaanika jeuri

Inatoka Uk. 6

“Kukua kwa biashara ya nje kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji ni eneo jingine lililofanikiwa kwani mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, yaliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 8.83 kwa kipindi cha miezi 12 iliyoishia Novemba, 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 16.5 kwa kipindi kilichoishia Machi, 2025,” alibainisha.

Profesa Kitila, alisema ongezeko hilo lilichagizwa kwa sehemu kubwa na mauzo ya bidhaa za madini, hasa hasa dhahabu na kwa upande mwingine zao la korosho na kuimarika kwa shughuli za utalii kulikochangiwa na utangazaji wa filamu za The Royal Tour na Amazing Tanzania.

Profesa Mkumbo aliyataja mafanikio mengine kuwa ni kuongezeka kwa Bajeti ya Serikali kutoka shilingi trilioni 34.88 mwaka 2020/21 hadi shilingi trilioni 57.04 mwaka 2025/26 na hivyo kuwezesha kuboresha huduma na miundombinu katika sekta mbalimbali zikiwamo afya, maji, elimu, nishati, ujenzi wa barabara, madaraja na treni ya kisasa ya SGR, pamoja na ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

Katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025, Profesa Kitila alisema, serikali ilifanya

marejeo ya kanuni za fedha za kigeni za mwaka 2022 kwa lengo la kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa fedha za kigeni nchini.

Vilevile, alisema serikali ilifanya mapitio ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, sehemu ya 26 ili kuhakikisha sarafu ya shilingi ya Tanzania inatumika katika upangaji wa bei na malipo ya bidhaa na huduma mbalimbali ndani ya nchi.

“Kutokana na jitihada hizo, mafanikio mbambali yamepatikana ikiwamo kiwango cha fedha za kigeni kuendelea kubaki ndani ya lengo la nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne ambapo hadi Machi, 2025, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani bilioni 5.69...”

“Kiwango hicho, kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 4.76, mwishoni mwa mwaka 2020,” alisema.

Katika kupunguza changamoto zilizojitokeza kutokana na uhaba wa dola ya Marekani, alisema serikali imeendelea kubuni mikakati mipya ya kuongeza wigo wa vyanzo vya akiba ya fedha za kigeni ikiwamo kufanya marejeo ya sheria ya ongezeko la thamani kwa kufuta tozo ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Benki Kuu.

Inaendelea Uk. 8

Habari Kuu



Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akifurahia jambo wakati wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM uliofanayika Dodoma juzi.

CCM yaanika jeuri

Inatoka Uk. 7

Vilevile, serikali imeanzisha programu ya ununuzi wa dhahabu ndani ya nchi kwa kutumia shilingi ambapo hadi Machi, 2025 takribani tani 3.42 za dhahabu yenye thamani ya Dola za Marekani, milioni 342.64 zilinunuliwa na kuhifadhiwa.

“Pia, ununuzi wa dhahabu ndani ya nchi, umewezesha uwepo wa soko la uhakika la dhahabu kwa wachimbaji wadogo waliojirasimisha pamoja na kuongeza wigo wa akiba ya nchi na hivyo kuilinda nchi na misukosuko ya kiuchumi.

Mikopo na madeni

“Kuongezeka kwa mikopo ya kigeni kwa sekta binafsi kutoka Dola za Marekani bilioni 5.34 Novemba, 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 7.38 Machi, 2025, kumewezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi hasa katika sekta za uchimbaji wa madini, fedha na bima, viwanda, usafirishaji na mawasiliano,” alifafanua.

Katika hatua nyingine, alisema Serikali imefanikiwa kulipa madeni yaliyohakikiwa ya shilin-

gi trilioni 4.40 kwa wakandarasi, watumishi, wa-toa huduma na wazabuni.

Katika eneo la kukuza uwezeshaji kiuchumi, alisema Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na juhudi hizo zilizumuisha utekelezaji wa sera, sheria, mikakati, programu na huduma mbalimbali za uwezeshaji.

“Mafanikio yaliyopatikana katika eneo hilo ni pamoja na kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa kupitia mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kutoka shilingi bilioni 904.25 mwaka 2021 hadi trilioni 3.5 mwaka 2024.”

“Kuongezeka kwa wananchi waliopata mikopo kupitia mifuko na programu za uwezeshaji kutoka wanufaika 3,562,810 mwaka 2021 hadi wanufaika 6,183,835 mwaka 2024 na kuongezeka wananchi waliojengewa uwezo wa uzalishaji na urasimishaji wa biashara katika sekta mbalimbali kutoka wananchi 3,829,412 mwaka 2021 hadi wanufaika 5,493,580 mwaka 2024.

“Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa marejesho ya mikopo kutoka mifuko na programu za uwezeshaji kutoka marejesho ya shilingi 501.73 bilioni mwaka 2021 hadi kufikia marejesho ya shilingi 2.17 trilioni mwaka 2024 pamoja na kuongezeka kwa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi kutoka vituo 11 hadi vituo 29 mwaka 2025,” alisema

Mpango wa kunusuru kaya maskini

Akizungumzia mikakati ya kuzisaidia kaya maskini, Profesa Kitila alisema Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini awamu ya tatu kwa maeneo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar na kwamba mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa kaya za walengwa kutoka 876,440 waliopata shilingi bilioni 34.9 mwaka 2021 hadi walengwa 1,371,916 waliopata shilingi trilioni 1.12 mwaka 2025.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

Kwa mujibu wa Profesa Mkumbo, serikali imeendelea kuratibu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 ambapo rasimu ilizinduliwa Desemba 11, 2024 na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema maandalizi ya rasimu hiyo yalikuwa jumuishi na shirikishi ambapo jumla ya washiriki 1,172,106 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walitoa maoni yao.

TMC, PIN wasisitiza uhuru kidijitali

Mkurugenzi wa Shirika la Tanzania Media Convergency (TMC), Asha Abinalah (kulia), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Paradigm Initiative kutokea Nigeria, Gbenga Sesanna (katikati) pamoja na Miriam Wanjiru - Ofisa wa Mipango kwa Afrika Mashariki Shirika la Paradigm Initiative katika mkutano na waandishi wa habari Ijumaa iliyopita jijini Dar es Salaam. (Picha na Mpiwapicha Wetu).



Na Mwandishi WETU

MASHIRIKA mawili yanayojihusisha na haki za kidijitali ya Paradigm Initiative (PIN), Nigeria na Tanzania Media Convergency (TMC), Tanzania yametoa mapendekezo kwa Mamlaaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kurejesha kikamilifu huduma ya Mtandao wa X (zamani Twitter).

Pia mashirika hayo yamehimiza kupatikan kwa huduma za na intaneti kwa ukamilifu wakati Tanzania ikijiandaa kuingia mchakato wa uchaguzi mkuu baadaye mwaka huu.

Mapendekezo hayo yalitolewa wiki iliyopita - Mei 29, 2025 jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa TMC, Asha Abinalah kufuatia Serikali ya Tanzania kuzuia upatikanaji wa mtandao wa X (zamani Twitter).

Asha alizungumza hayo baada ya kumalizika kwa warsha ya siku mbili ya "Digital Rights and Elections in Africa Monitor (DREAM) - Toleo la Tanzania," ulioangazia vitisho vinavyojitokeza na vikwazo dhidi ya matumizi ya intaneti.

Alisema haki za watumiaji wa intaneti zinapaswa kulindwa wakati wote bila kujali kuwepo kwa mazingira gani.

Alipendekeza pia TCRA kuepuka kufuta au kuzima majukwaa ya vyombo vya habari mtandaoni na kuhakikisha uhuru wa kujieleza mtandaoni na nje ya mtandao, hasa kwa wanahabari, wanasiasa, na sauti za kiraia kama inavyolindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

nia.

Pamoja na hayo alipendekeza kutangaza taarifa za uchaguzi kwa njia rahisi na hata ikiwezekana kwa lugha za wenyeji.

Alieleza kuwa Watanzania wanapendekeza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAJG), kufuatilia hali ya haki za kidijitali wakati wa mchakato wa uchaguzi na kuripoti ukiukwaji kwa uwazi.

Kadhalika kwa kushirikiana na asasi za kiraia alipendekeza tume hiyo kuongeza uelewa kuhusu matumizi bora ya mitandao.

Kwa upande wa kampuni za mawasiliano, alizitaka kuhakikisha utulivu wa mitandao na uwazi kuhusu maagizo yoyote kutoka serikalini kwa kutoa taarifa kwa umma na kuchapisha ripoti za uwazi mara kwa mara kuhusu maombi ya serikali kuhusu maudhui au upatikanaji wa taarifa. Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Paradigm Initiative Gbenga Sesana alisema Mpango wa DREAM ni sehemu ya mradi wa Afrika unaoratibiwa na Paradigm Initiative kufuatilia, kuhifadhi kumbukumbu, na kujibu ukiukwaji wa haki za kidijitali katika vipindi vya uchaguzi.

Alisema Tanzania, nchi inayojipambanua kuheshimu uhuru wa kujieleza na ustawi wa matumizi ya intaneti, inapaswa kuhakikisha kwamba haki ya matumizi ya mitandao, haiingiliwi na chombo chochote kuanzia sasa na hasa wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Tafakuri ya BagonzaNa Dkt. Benson
BAGONZA

Wakili Peter Madeleka, akizungumza na wafanyabiashara waliopoteza mali zao katika jengo lililoporomoka eneo la Kariakoo baada ya kesi yao ya kudai fidia ya shilingi bilioni 40, kuahirishwa kutokana na changamoto ya kiafya ya Jaji anayeendesha kesi hiyo katika Mahakama Kuu ya Ardh, jijini Dar es Salaam juzi.
(Picha na Fidelis Felix)

Nguvu na akili: Tubomoe au tujenge?

KUNA mwimbaji aliimba; “Bomoa eh, bomoa baba tutajenga kesho.”

Pia wapo wana mikesha wakaimba; “Chocheaa, chocheaa karama ya Bwana chochea.”

Lakini, Bwana Yesu anasema katika Mathayo 5:9 – kwamba; “Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu.”

Nchi yetu sasa ina joto kali. Tunahitaji kiyoyozi cha kupoza, siyo heater ya kuongeza joto.

Anayehisi joto kali na anayehisi baridi kali, nani anahitaji kutumia akili kujilinda?

Mwenye joto kali aweza kuvua nguo zote na kubaki uchi ili asisumbuke kwa joto.

Mwenye baridi anahitaji akili kupata nguo za joto ili kujilinda kwa baridi.

Tukiwa taifa, kwa sasa tunahitaji akili siyo nguvu. Nguvu ni kwa ajili ya kubomoa, lakini akili ni kwa ajili ya kujenga.

Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu, hao wana harakati wa Kenya hawakutumwa na serikali yao. Mnaharibu uhusiano wa nchi kwa ujinga wa watu wachache.

Kwamba wanaojibu kwa kukashifu Wakenya, hawajatumwa na rais wala serikali. Uchawa usivuruge uhusiano na nchi jirani.

Kwamba, huyo Gwajima kajituma au katumwa, anajua yeye. Jadilini hoja achana na hicho kinachodaiwa kuwa ukichaa wake.

Mlipoiba kura ili ashinde hamkujadili bungeni, leo bunge linafika mwisho ndo mnatumbia mliiba kura? Basi futeni sheria zooote al-

izoshiriki kutunga. Hatutaki sheria zilizotungwa na mwizi?

Haya sawa, Gwajima kakosa adabu. Nyie mmekosa zaidi kwa kujitambulisha mlivyo wezi.

Ileweke kwamba rais wetu siyo “Katope” kwamba mnamkinga na mvua asiyeyuke. Mbona mnamsengeny kila siku mitaani?

Kiongozi wetu ana uwezo mkubwa tunamjua na hilo mnalijua. Ana roho ya utu na tunaijua. Msimtumie kubariki mambo mabaya yanayotokea.

Itambulike kuwa kutekwa na kupotea kwa watu ni tatizo. Kama kuna aliyeteka kwa kugizwa na mamlaka, ajitokeze tumuone. Kimya hakiondoi tatizo.

Shetani Gwajima kahoji jambo jema. Tulikatae kwa sababu limeletwa na shetani? Mamlaka ya kutoa roho tumwachie Mungu aliyeiweka (Mwanzo 2:7).

Sasa kwa nini Msajili anaipigia kampeini Chadema? Kila hatua anayochukua, inachochea moto na kuongeza huruma kwa chama hicho cha upinzani.

Ugaidi na uhaini wa Chadema hauongezi uzalendo kwa vyama vingine. Chadema ina uwezo wa kujiharibia na tunauona bila darubini. Iache ijifie.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Na Godwin CHILEWA,
Houston

Kurunzi la Intelejensia

Bunge letu lijitafakari zaidi



TUKUBALI au tusikubali, wakati umefika sasa kwa Bunge la Jamhuri ya Tanzania kujitafakari na kuchukua hatua ili lizidi kuheshimika zaidi.

Hivi sasa bunge letu ni kama limeacha kushughulika na hoja nzito kulisaidia taifa na watu wake, na kujikita kwenye mipasho na malumbano yasiyosaidia masikini.

Tukio la karibuni kabisa linalothibitisha hali hii ni mjadala uliozuka bungeni kufuatia hoja ya Mbunge Josephat Gwajima kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu na utekaji. Pia udhalilishaji wa raia wa Kenya waliokuja nchini kushiriki katika kesi ya Tundu Lissu.

Badala ya kuchambua kwa kina hoja zilizotolewa, wabunge wengi walijikita katika kumdhahaki Gwajima na “kumtetea” rais kwa jazba zisizo na mantiki wala mshiko wa kisheria au kimaadili.

Kwa masikitiko makubwa, baadhi ya wabunge waliochangia hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani walifikia hatua ya kusifia vitendo vya udhalilishaji vilivyowakumba Martha Karia na Boniface Mwangi — raia wa Kenya waliokuja Tanzania kufuatilia haki — huku wengine wak-

ishangazwa kwanini “hawakuuawa.”

Hii siyo tu fedheha kwa taifa, bali ni doa jeusi katika historia ya Bunge ukiwa ni mhimili unaopaswa kuwa nguzo ya haki, ulinzi wa katiba na utetezi wa watu wote bila kujali uraia wao.

Kimsingi, Bunge linapaswa kuwa chombo makini katika utendaji wake, lakini bunge letu sasa ni kama halifanyi kazi kwa weledi, na halizingatii matakwa ya wananchi.

Tena kwa muda mrefu tumeshuhudia ubwete na upendeleo wa kisiasa (Bias) ukitawala. Ingawa Bunge ni chombo cha wananchi kinachopaswa kufanya kazi zake kwa kuangalia maslahi mapana ya taifa, Bunge la Tanzania limejivua utaifa na kujivika uchama.

Mara nyingi wabunge wa chama tawala hujikita kulinda maslahi ya chama na viongozi wake kuliko maslahi ya wananchi.

Mbunge anapojaribu kutoa hoja inayokosoa mamlaka, hujibiwa kwa kejeli, dharau au hata vitisho. Hili linajidhihirisha katika mjadala unaoendelea kuhusu kauli ya Askofu Josephat Gwajima.

Badala ya kujadili hoja zake, wabunge wamejikita kutoa kauli za kujipendekeza kwa viongozi bila kuchambua chanzo halisi cha kauli ya Gwajima.

Mbaya zaidi ni kwamba serikali ya chama tawala imegeuza Viti Maalum kuwa mashine ya kupitisha ajenda zake.

Ileweke kuwa nafasi za viti maalum ziliwekwa kwa lengo la kuongeza makundi maalum bungeni kwa manufaa ya taifa. Hata hivyo, wabunge wa viti hivyo wamegeuka kuwa mwiba kwa wananchi.

Wabunge hawa mara nyingi wamekuwa kama kura za mkononi kwa serikali, pasipo msi-mamo huru au mchango wa kitaaluma.

Hawa wanapotosha dhana ya uwakilishi wa wanawake kwa kuwa wengi wao huteuliwa kwa misingi ya uaminifu wa kisiasa, urafiki na kujua-na, wala siyo uwezo au weledi wa mhusika.

Pengine matatizo yote haya yanatokana na baadhi ya wabunge kutokuwa na elimu au uwezo wa kuchambua sera.

Kurunzi la Intelejensia

Bunge letu...

Inatoka Uk. 11

Ni ukweli ulio dhahiri kuwa wabunge wengi hawana elimu ya kutosha wala uwezo wa kuchambua miswada ya sheria au hoja za msingi.

Wengine wana elimu ya vyuo vikuu lakini hawana elimu ya bunge, sheria wala diplomasia, huku wengine wakiwa na elimu ya chini mno, hata darasa la saba kabisa!

Hii imesababisha hoja nyingi muhimu kupuuzwa au kufanyiwa uamuzi bila mantiki ya kina.

Baadhi ya wabunge hufanya mizaha, na kuropoka mambo mazito yanayoathiri taswira ya nchi kimataifa.

Mapendekezo ya mabadiliko

Ili kurejesha heshima, mamlaka na tija ya Bunge la Tanzania, yafuatayo yapaswa kufanyiwa kazi; kwanza kabisa ni mabadiliko ya katiba yatakayolipa Bunge uhuru kamili ukiwa mhimili wa dola unaojitegemea, bila kuingiliwa na serikali au chama tawala.

Viongozi wa Bunge, hususan Spika na Naibu Spika wachaguliwe kwa uwazi na kwa misingi ya sifa na weledi, siyo uaminifu kwa chama pekee, kujuana, au kulipa fadhila.

Pili, ni muhimu iundwe Tume Huru ya Kikatiba kwa ajili ya mchakato wa katiba mpya inayoweza msingi imara wa mgawanyo wa mada-raka na uhuru wa mihimili.

Tatu, yafanyike marekebisho ya kikatiba na sheria kufuta nafasi za ubunge wa viti maalum. Wabunge hawa wamekuwa nyenzo ya kisiasa ya kupitisha ajenda, na siyo chombo cha uwakilishi wa kweli bungeni.

Nne, sheria ibadilishwe kuweka kiwango maalum cha elimu kwa wagombea ubunge: Ingefaa sana liwekwe sharti kwamba mgombea wa nafasi ya ubunge awe angalau na shahada ya kwanza.

Tano, ziundwe Kamati Huru za Uchunguzi na Uwajibikaji: Kamati za Bunge ziwe na mamlaka ya kweli ya kuchunguza malalamiko ya wananchi na kuchukua hatua bila hofu wala upendeleo.

Hoja kama zile zilizotolewa na Gwajima kuhusu haki za binadamu, zilipaswa kufanyiwa uchunguzi rasmi, na kutolewa majibu siyo kupuuzwa kwa jazba na kujipendekeza.

Pamoja na hilo ni muhimu pia kila mbunge ahudhurie mafunzo ya uongozi, maadili ya umma, na usimamizi wa sheria kabla ya kuanza rasmi kazi za kibunge.

Wabunge wengi wa sasa hawazingatii maadili ya nafasi yao, hawatimizivwajibu wao kwa weredi, na wamegeuka kuwa chawa wa mama na chama tawala. Hili ni tatizo kubwa linalopaswa kutatuliwa mara moja.

Mwenendo wa sasa wa Bunge ni dalili ya mifumo iliyokufa kiuhuru, kifikra, na kimaadili.

Kushangilia udhalilishaji wa binadamu, kusia vitisho vya kifo dhidi, na kupuuza hoja nzito za kitaifa siyo tu aibu, bali ni hatari ya kiusalama wa ndani na wa kimataifa.

Ni wakati wa wananchi, asasi za kiraia, na viongozi wa kweli kusimamia mapambano ya mabadiliko ya katiba, kufuta viti maalum, kuweka viwango vya kielimu, na kurejesha heshima ya mhimili huu muhimu wa nchi.

Bunge la kweli linapaswa kuwa sauti ya watu, siyo kinga ya mamlaka.



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Tuzo Maalum ya Heshima ya Bunge kutoka kwa Spika wa Bunge la Dk. Tulia Ackson katika hafla iliyofanyika viwanja Bunge, jijini Dodoma, (mwishoni mwa wiki. Picha na Ikulu)

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Hili ndilo Bunge, ubunge, wabunge wetu

BAADA ya kufuatilia baadhi ya mijadala ya Bunge wiki iliyopita, niliona kuna sababu ya kujiangaliza kidogo kwa nini tunalo Bunge, muundo wake, kazi zake na pia kujikumbusha kuwa Bunge la Tanzania haliko hewani, ni sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika.

Nilipofuatilia mjadala kwenye bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, walikuwepo baadhi ya wabunge waliojadili kwa kuangaliza mambo yaliyotokea kwa kurudishwa kwao raia wa Kenya waliofika nchini Tanzania kusikiliza kesi ya uhaini iliyokuwa ikiendelea dhidi ya Tundu Lisusu.

Mfano mmoja ni mbunge aliyesema kuwa yule aliyerejeshwa kwao ilibidi awe ameumizwa kiasi cha kurudishwa akiwa anapumulia mashine.

Pia yupo aliyesema vyombo vyetu vya dola viwashughulikie hao 'kenge wa ndani na wa nje ya nchi,' akimaanisha raia wale wa Kenya waliofika wana watu kama wao wanaofuatilia kesi hiyo hapa nchini ambao yeyé aliwaita kenge.

Kwa kauli kama hizi tu, bila kujaribu kufuatilia mengi yaliyojadiliwa, nilitamani kujua iwapo wabunge hawa wanajua vizuri Bunge na ubunge wao kwa mujibu wa Katiba.

Nikiangalia ibara ya 63 [2] ya Katiba inaelezea vizuri madaraka ya Bunge kwa sehemu yake ya pili kuwa:

“(2) Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.”

Kwa mujibu wa ibara hii, Bunge kupitia wabunge linapaswa kuisimamia serikali kwa niaba ya wananchi.

Mbunge anapotoa kauli ya kuwaita wananchi kenge, inanipa wasiwasi iwapo mbunge huyo anaelewa nafasi yake hapo bungeni na kuwa uwepo wake ni kwa niaba ya hao hao anawaita kenge?

Kazi nyingine ya Bunge ni kushauri, sasa inashangaza kwamba tunamsikia mbunge akiishauri serikali katika utekelezaji wake iumize watu.

Ushauri wowote unatakiwa kuwa kwa mujibu wa Katiba. Mbunge huyu ametumia ibara gani ya Katiba inayotaka mtu anayerejeshwa kwao kwa sababu yoyote ile, aumizwe na kushughulikiwa kwa maana hiyo hiyo ya kuumizwa?

Hizi kauli zilileta shida kwa waliozisikia na huko nchi jirani ambako raia wao ndiyo waliorejeshwa, ilibidi wakague tovuti ya bunge letu kujua aina ya wabunge tulionao.

Licha ya kauli hizi kukiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia ni kinyume cha mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo Tanzania ni mmoja wa wanachama wake.

Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki una misingi mikuu sita mmojawapo ukiwa ni utawala bora unaojumuisha misingi ya demokrasia, utawala wa sheria uwajibikaji, uwazi, haki jamii, usawa, pamoja na kutambua, kukuza na kulinda haki za binadamu na haki za watu kwa mujibu wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Haki za Watu.

Katika mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki misingi ya utekelezaji wake unaelekeza kuwa unapaswa kuongozwa na dhana ya kuwatanguliza watu (People_centered).

Wabunge wetu wanajua kuwa wana wajibu wa kufuata miongozo hii kabla hawajawaita watu wa Afrika Mashariki wanaofanya wajibu wao kuwa ni kenge na pia kushauri watendaji kudhuru watu.

Ni vyema Bunge letu liongozwe kwa mujibu wa Katiba na siyo vinginevyo na wabunge hawawezi kujiondoa kuwa Bunge.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337 240.

Habari

Mkakati wa CCM kuvuta kura



Maspika wastaafu, Job Ndugai (kushoto) na Anna Makinda (kulia) wakiwa kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, Dodoma juzi.

Na Waandishi WETU, Dodoma

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimezindua ilani itakayokiongoza wakati wa uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu, ili kutafuta idhini ya wananchi kuongoza nchi kwa mara nyingine.

Ilani hiyo mpya iliyozinduliwa Ijumaa Mei 30, 2025 inasimamia maeneo manane ya kimkakati ambayo yatapelelele kipaumbele kuanzia mwaka huu 2025 hadi 2030 kwa kutumia kauli mbiu ya 'Kazi na utu, tunasonga mbele.'

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, ndiye aliainisha maeneo hayo ya kimkakati mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM uliomalizika Ijumaa Mei 30 mwaka huu 2025.

Katika maelezo hayo, Profesa Mkumbo alisema ilani hiyo inalenga kukiongoza chama hicho kuunda serikali ambayo itachochea mapinduzi ya uchumi wa kisiasa, fungamanishi, jumuishi na shindani, uliojengwa katika msingi wa kuongeza thamani rasimali zilizozalishwa nchini.

Sekta binafsi

Kuhusu sekta binafsi, alisema CCM inatarajia kuimarisha sekta hiyo kwa kuanzisha mfuko maalum wa kuwezesha upatikanaji wa mitaji hususani kwa wajasiriamali wa biashara ndogo, za kati na kampuni changa.

Pia Profesa Mkumbo aligusia miundombinu ya umwagiliaji na kusema chama hicho kimepanga kuongeza miundombinu ya sekta hiyo kwa ajili ya kuongeza kilimo cha umwagiliaji pamoja na kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora na kwa bei nafuu na kutoa ruzuku ya pembejeo.

Kuhusu ajira kwa vijana, alisema CCM inatarajia kuzalisha idadi ya ajira kwa vijana katika sekta rasmi na isiyo rasmi na kwamba idadi ya ajira zinazotarajiwa kuzalishwa hadi 2030 ni milioni 8.5.

Na kuhusu vituo vya uwezesaji kiuchumi, alisema vitaanzishwa vituo katika mikoa ili kusogeza huduma kwa wananchi na kuimarisha utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini (Tasaf).

Inaendelea Uk. 15

Mkakati wa CCM...

Inatoka Uk. 14

“Katika kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii, CCM inatarajia kuongeza fursa za elimu kwa kuendelea kutoa elimu bila ada kuanzia elimu ya msingi hadi sekondari...”

“Kuhusu maslahi ya walimu, serikali ya CCM itapitia upya maslahi ya walimu na kuyaboresha ipasavyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi na nyumba za walimu...”

“Kwa upande wa elimu ya msingi, serikali itaimarisha elimu ya ufundi stadi kwa kujenga vyuo vipya vya elimu ya ufundi na mafunzio ya ufundi stadi,” alisema Profesa Mkumbo.

Aidha, kuhusu afya alisema Serikali ya CCM itawezesha wananchi wote kujiunga na bima ya afya na kwa upande wa sekta ya maji alisema itaongeza idadi ya kaya zilizofikiwa na huduma za maji safi na salama kwa asilimia isiyopungua 90.

Ilani hiyo pia imeainisha kuwa serikali itapunguza gharama za vifaa vya ujenzi ili kuwezesha wananchi husiusani wa kipato cha chini kujenga nyumba bora za kisasa na kwa gharama nafuu.

Pia, serikali itaendelea kuboresha makazi mijini kwa kuhakikisha makazi, nyumba na majengo yote yanarasimishwa kwa kupimwa, kupangwa na kumilikisha.

Usafiri na usafirishaji

Ilani hiyo imeainisha kuwa itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji.

Profesa Mkumbo aligusia barabara na mada-raja ambapo alisema lengo ni kuunganisha kwa kiwango cha lami barabara za makao makuu na wilaya, kuhakikisha barabara zote za vijijini zinakarabatiwa na kujengwa ili ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka, kuanza ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya barabara maeneo ya Morocco, Mwenge, Magomeni na Tabata jijini Dar es Salaam.

“Serikali itakamilisha miradi ya ujenzi wa madaraja inayoendelea, ujenzi wa barabara kubwa za kuunganisha mikoa na nchi jirani, kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya nne mpaka awamu ya sita jijini Dar es Salaam...”

“Ujenzi wa reli ya standard gauge utaendelea katika mikoa mbalimbali nchini, kujenga reli na kuweka usafiri wa mijini katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma ili kuepusha msongamano na kurahisisha usafiri, kujenga reli ya kisasa ilki kuunganisha bandari ya Tanga kuelekea Arusha hadi Musoma,” alisema Profesa Mkumbo.

Kwa upande wa bandari, alisema wanatarajia kujenga bandari mpya ya Bagamoyo, kuboresha bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Kigoma, Kalema, Musoma na bandari kavu katika eneo la Kurasini, Dar es Salaam, Kwala mkoani Pwani na Ihumwa, Dodoma.

Kwa upande wa meli, ilani inaahidi ukarabati wa meli zilizopo katika maziwa makubwa na kujenga meli mpya za mizigo na abiria katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa na katika Bahari ya Hindi.

Ndege zaidi kununuliwa

Kwa upande wa usafiri wa anga, alisema zitanunuliwa ndege nane na kuendelea kuimarisha shirika la ndege la Tanzania.

Katika kukuza matumizi ya sayansi na teknolojia, alisema serikali itaandaa na kutekeleza mkakati maalum wa kutumia teknolojia zinazoibukia ikiwamo akili unde, matumizi ya roboti, satelaiti, block chain, kuimarisha ufanisi na tija katika uzalishaji na utoaji wa huduma.

“Kuongeza wigo wa wananchi wa vijijini kutumia teknolojia ya habari ili kunufaika na fursa zitokanazo na shughuli za uzalishaji kiuchumi na kijamii,” alisema.

Michezo

Kuhusu utamaduni wa taifa, Ilani hikyo imeainisha kuwa itaongeza jitihada za kuitangaza lugha ya Kiswahili kimataifa, ambapo pia serikali itaweka mfumo imara wa kulinda haki miliki za wasanii kwa kuimarisha sheria za haki miliki ili kuhakikisha wasanii wananufaika na kazi zao.

“Pia kutajengwa kituo kikubwa cha burudani (arena) kwa ajili ya maonyesho ya kazi za sanaa na burudani nyingine kitaifa na kimataifa...”

“Pia kuanzisha na kuendeleza shule za michezo kwa lengo la kuandaa wanamichezo wa leo na baadaye, kujenga viwanja vya michezo vya kisasa vyenye viwango vya FIFA na Olympic (Afcon City Arusha),” alisema.

Habari

Vuta nikuvute Takukuru vs Dkt Mollel

Na Rachel MRISHO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kilimanjaro inachunguza tuhuma zilizotolewa na Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Siha, Dkt. Godwin Mollel, kuwa taasisi hiyo imeshindwa kubaini wizi jimboni humo.

Wakati mbunge huyo akiituhumu Takukuru kwa madai ya kushindwa kazi, lakini hata yeye anahusishwa na tuhuma za rushwa.

Taarifa zilizopo zinadai kuwa hivi karibuni Mbunge huyo alitoa shilingi 60,000 kwa kila mwenyekiti wa kijiji katika jimbo hilo lenye vijiji 60, kitendo ambacho kimetafsiriwa kuwa ni hongo.

Akizungumza na Pambazuko, mkuu wa Takukuru mkoani humo, Musa Chaulo, amesema wapo kwenye uchunguzi wa masuala hayo.

“Suala hili siwezi kulizungumza kwenye simu, ni kitu ambacho kipo kwenye uchunguzi kwa sasa,” amesema Chaulo kwa ufupi.

Dkt. Mollel ametupa lawama kwa Takukuru akidai kuwa imeshindwa kubaini wizi wa fedha takribani shilingi milioni 133, badala yake kazi hiyo imefanywa na madiwani.

Akizungumza kwenye mkutano na wenyevidi wa vijiji katika Ukumbi wa Hospitali ya Kibongoto, iliyopo Kata ya Siha Mashariki, wilayani Siha, mbunge huyo alitamka kuwa; “Takukuru imeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.”

“Wameshindwaje kupata taarifa ya wizi wa fedha shilingi milioni 133 mpaka madiwani ndio wanakuja kugundua hata wao hawajui, sijui kama mnanielewa ...”

“Ninasema hivyo ili isikike kwa sababu ninajua hata hapa kuna watu wananirekodi, maana simu yangu inaonyesha nani anarekodi...”

“Wale... wawapelekee jamaa wa usalama wawaambie Mollel amesema acheni Ba...(wenyevidi wanamalizia kwa kusema bangii...). Fanyeni kazi la sivyo nitawaingia na nyie nitawanyoosha yaani tunaibiwa tu hela hamuoni...”

“Wamemuita mtu mmoja Takukuru, hatu-

katai mtu kuitwa Takukuru, inawezekana kuna kitu kweli cha kisheria, lakini tunataka hiyo nguvu inayotumika kwenye siasa mara kuwaita madiwani Takukuru mara mbunge, sijui kafanya nini mnamuita Takukuru tunataka hiyo nguvu ielekezwe kwenye miradi yetu,” alisema Dkt. Mollel.

Katika kikao chake na madiwani, Dkt. Mollel aliwapatia fedha wenyevidi hao na kabla ya mgao huo aliwaambia; “Tuliona bill (ankara) ya chakula ni kubwa, tukaona acha tugawane shilingi elfu sitini, sitini kwa sababu kuna waliotoka mbali ila wanaweza wasione thamani, lakini haki ya Mungu si mmepata nauli ya kuja kumuona ndugu yenu, niko na afya njema.”

Akizungumza na Pambazuko mmoja wa wenyevidi hao ambaye hakutaka jina lake litajwe alikiri kupokea fedha hizo na kueleza kuwa haikuwa nyakati nzuri kwa mbunge huyo kugawa fedha hizo.

“Mbunge wetu alitugawia fedha shilingi 60,000 kwa kweli alitupa kama nauli, tulikuwa wenyevidi wa vijijini 60 kila mmoja alipewa. Hakuna mtu anaweza kukataa pesa, sisi wenyevidi hatulipwi mshahara...”

DK. Mollel ametafutwa mara kadhaa kupitia simu yake, lakini hapokei na hata akipelekewa ujumbe wa simu, hajibu.



Mbunge wa Siha, Dkt. Godwin Mollel.

Mkutano Mkuu CCM zaidi ya siasa



*Nabii na Mtume
wa Kanisa la
Inuka Uangaze,
Boniface
Mwamposa,
akiwa kwenye
mkutano mkuu
wa CCM juzi.*

Na Arodia PETER, DODOMA

MKUTANO Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) uliomalizika Ijumaa iliyopita Jiji la Dodoma ulikuwa ni zaidi ya jumuiko la kisiasa la chama hicho tawala.

Mkutano huo maalum, pamoja na kujumuishwa wajumbe halali zaidi ya 1,900 – pia ulikutanisha watu wa kada mbalimbali wasiokuwa waalikwa rasmi; wafanyabiashara, wakulima, wanafunzi na hata wageni kutoka nje wenye malengo ya kufanya uwekezaji.

Pia idadi kubwa ya wageni ilikuwa ni wanasiasa wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za kuchaguliwa au kuteuliwa na CCM kuwania ubunge, uwakilishi (Zanzibar) na hata udiwani.

Hawa walifika Dodoma kwa ajili ya kukutana na “wakubwa” wa Serikali ya Tanzania na CCM, ambao ndio wanafanya maamuzi kuhusu mambo mengi nchini.

Kuwa Dodoma katika kipindi hicho kuna urahisi wa kukutana na watoa uamuzi na haku-na mlolongo wala itifaki za kufuata kuonana na wakubwa hao.

Pia, kusanyiko hilo lilikuwa fursa kubwa kwa wafanyabiashara wa nyumba za wageni, wafanyabiashara wa vyakula na huduma zingine, kwani Dodoma ilifurika wageni ambao walihitaji huduma hizo.

Wenye kusaka fursa mbalimbali ilikuwa rahisi mno kuwakuta mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi na maofisa wa taasisi na idara mbalimbali na kuzungumza nao.

Pambazuko limebaini kuwa mkutano huo maalum wa CCM ulivuta takribani wageni 5,000 ambao waliifanya Dodoma ionekane imefurika.

Wengi wa hao hawakuwa wajumbe halali wa Mkutano huo na mtu unaweza kujiuliza hawa ambao si wajumbe wamefuata nini Dodoma?

Tukizungumzia mkutano mkuu wa chama hicho uliomalizika mwishoni mwa wiki, baadhi ya makundi yakiwamo ya wanasiasa, wafanyabiashara na madalali wao walitumia kusanyiko hilo kujipatia manufaa.

Nje ya Ukumbi wa Jakaya Kikwete ulipofanyika mkutano huo paligeuzwa maonyesho ya bidhaa mbalimbali. Mabanda mbalimbali ya wajasiliamali wa nyama choma, chakula, vinywaji, taasisi za fedha walitumia fursa hiyo kufanya biashara na wengine kunadi bidhaa zao.

Wapambe wa wanasiasa wanaojipanga kugombea nafasi za ubunge walikuja kwa lengo la kukutana na wajumbe kuweka mazingira rafiki ya kukumbukwa wakati wa upitishwaji wa majina ya wagombea kwenye vikao vya halmashauri kuu na kamati kuu za chama.

Kwa kuwa baadhi ya wajumbe wa mkutano mkuu wa CCM ni wafanyabiashara wakubwa nchini, watu wengine walikuja kwa malengo ya kuomba misaada ya kifedha, matibabu kwa wafanyabiashara na viongozi wa chama na serikali.

Wafanyabiashara mbalimbali walikuwa kwenye eneo la mkutano kwa lengo la kutafuta ‘connection’ za kibiashara kwa wakuu wa taasisi za serikali waliokuwa wanahusika kwa namna moja ama nyingine kwenye mkutano huo.

Pia watu mbalimbali wanakwenda kwenye mkutano mkuu huo ili kupata nafasi ya kukutana na wakuu wa taasisi nyeti za serikali, wakiwamo wakuu wa wilaya, mikoa, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, sekta binafsi na watu wengine maarufu wakiwamo wasanii.

Wanadada wanaofanya biashara ya kuuza miili yao nao hawakuwa nyuma kwani walionekana kwenye viunga hivyo wakitarijia kusaka wateja kupitia jumuiko hilo.

Mkutano mkuu maalum wa CCM uliofanayika ukumbi wa Jakaya Kikwete pia tunaweza kuiita kuwa ilikuwa ‘picnic ya kisiasa’ kwa watu kula, kunywa, kufurahi, na kujipatia fusa za maendeleo.



Uchumi & Biashara

Benki Afrika Kusini yashiriki ujenzi SGR



Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba

Na Benny MWAIPAJA, Abidjan

WAZIRI wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, ameishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA), kwa kushiriki katika ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).

SGR ni mradi ambao ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania na nchi jirani zitakazonufaika na mnyororo wa thamani wa mradi huo wa kika.

Dkt. Nchemba amesema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Buitumelo Mosako, pembeni ya Mikutano ya Mwaka ya Bodi ya Magavana wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) iliyofanyika Abidjan nchini Ivory Coast.

“Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati

kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini kwa mchango wenu muhimu katika kufadhili ujenzi wa SGR kipande cha tatu na cha nne (Makutupora hadi Isaka) kwa kiasi cha dola za Marekani milioni 100...”

“Zaidi ya hapo, tunatambua na kuthamini msaada wa kifedha wa kiasi cha dola za Marekani milioni 100 uliotolewa awali kwa ajili ya kujenga kipande cha pili, ambao uliweka msingi imara kwa mradi mzima wa SGR” alisema Dkt. Nchemba.

Kutokana na juhudi hizo za pamoja, Dkt. Nchemba alisema maendeleo ya ujenzi yamekuwa makubwa ambapo kipande cha kwana (Dar es Salaam hadi Makutupora) kimekamili kwa asilimia 99.63 na treni imeanza kufanya kazi rasmi Julai 2024, wakati kipande cha tatu (Makutupora hadi Tabora) ujenzi wake umefikia asilimia 14.53, na kipande cha nne (Tabora hadi Isaka) ujenzi umefikia asilimia 6.48.

“Kutokana na umuhimu wa mradi huu, nachukua fursa hii tena kuiomba benki yako iendelee kuunga mkono utekelezaji wa kipande cha sita na saba ya Reli ya Kisasa (SGR), ambavyo upatikanaji wake wa fedha za kutekeleza vipande hivyo unasimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB),” alisema.

Aliongeza kuwa Tanzania imefungua milango ya ushiriki wa sekta binafsi katika kuendesha mradi huo wa kimkakati ikiwemo uwekezaji wa mabewa na vichwa vya treni na kutoa wito kwa wawekezaji kuchangamkia fursa hiyo.

Aidha, Dkt. Nchemba aliishukuru Benki hiyo kwa kuonesha utayari wake wa kutaka kuwekeza zaidi katika maendeleo ya Tanzania katika sekta za elimu, maji, afya, ujenzi wa miundombinu pamoja na kilimo.

Kwa upande wake, Mosako alisema kuwa milango ya ushirikiano na Tanzania iko wazi na kwamba benki yake inasubiri kukamilika kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, ili waweze kuangalia maeneo ya kushirikiana.

Alisisitiza kuwa benki yake iko tayari kuwekeza zaidi Tanzania katika kusaidia miradi ya kimkakati na kijamii katika sekta za maji, afya, nishati, uchumi wa kidigitali, ujenzi wa makazi ya gharama nafuu na ujenzi wamiundombinu mbalimbali.

Biashara zinazochipukia zashamiri

Na Mwandishi WETU

TANZANIA imeendelea kushuhudia ongezeko kubwa la shughuli za ubunifu na ujasiriamali kupitia sekta ya biashara changa (startups), hali inayoashiria mabadiliko chanya katika mazingira ya biashara na maendeleo ya uchumi.

Ripoti ya Hali ya Biashara Zinazochipukia ya 2024, inaeleza kuwa idadi ya biashara zinazochipukia zilizosajiliwa nchini imeongezeka kwa asilimia 24 na kufikia 1,041 kutoka 842 mwaka 2023.

Pia kutokana na biashara hizo ajira 138,453 zimetengenezwa kupitia sekta hiyo, ongezeko la asilimia 23 ukilinganisha na mwaka uliopita.

“Biashara zinazochipukia zimezidi kuwa mhimili wa ubunifu, kuzalisha ajira na kuchochea mabadiliko ya kiuchumi na kijamii,” anasema Mwenyekiti wa Bodi ya Tanzania Startup Association (TSA), Paul Makanza.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, biashara nyingi zinazochipukia zimejikita katika sekta muhimu kama vile teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama), kilimo (AgriTech), afya (HealthTech), elimu (EdTech) na biashara mtandaoni (E-commerce).

Mwelekeo huu wa kidigiti umewezeshwa biashara hizi kutoa suluhisho bunifu kwa changamoto za kijamii na kiuchumi, hasa maeneo ya vijijini na mijini yenye huduma duni.

Hata hivyo, ripoti inaonyesha kuwa asilimia 66 ya biashara hizi zipo katika hatua za awali, zikihitaji msaada mkubwa katika kufikia hatua ya ukuaji na kupata masoko.

“Biashara zinazochipukia zilianza kutambuliwa rasmi kama moja ya vichocheo vya kukuza uchumi kupitia Dira ya Taifa ya 2050,” inabainisha ripoti hiyo.

Ripoti inabainisha pia kuwa kuna changamoto za upatikanaji wa mitaji ambazo zimeendelea kuikabili sekta hii.

Ingawa uwekezaji kutoka ndani ya nchi umeongezeka - hasa kupitia benki kama NMB iliyotoa zaidi ya dola milioni 36.8 – biashara nyingi zinazochipukia bado zinategemea zaidi ufadhili

kutoka kwa wawekezaji wa nje, hasa katika sekta ya FinTech na AgriTech.

Serikali, kwa kushirikiana na wadau kama TSA, imepitisha mikakati mbalimbali ikiwemo sera ya uchumi wa kidijitali, sera ya uwekezaji (2025–2035) na maandalizi ya mfuko wa uwekezaji wa mitaji hatarishi wenye zaidi ya dola milioni 40.

Pia, ripoti inaonyesha kuwa asilimia 75 ya biashara zinazochipukia zimesajiliwa rasmi, hatua muhimu kwa upatikanaji wa mikopo, fursa za soko na ushiriki katika sera za umma.

Hata hivyo, gharama na urasimu wa usajili vimeendelea kuwa kikwazo kwa asilimia 25 ya biashara ambazo bado hazijasajiliwa.

Lakini ripoti inasema kuwa ili mafanikio haya yawe endelevu, ni muhimu kuongeza uwekezaji katika elimu ya ujasiriamali, kurahisisha sera na masharti ya kibiashara, na kuimarisha mfumo wa usaidizi kwa biashara zinazochipukia kutoka hatua ya wazo hadi kufikia soko.

Kwa kufanya hivyo, Tanzania inaweza kujenga uchumi jumuishi unaotegemea ubunifu na ujasiriamali wa vijana wake.



Mwenyekiti wa Bodi ya TSA, Paul Makanza.

Habari

Kilichofanya Dkt Tulia kujitosa Uyole

Na Mwandishi WETU

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Tulia Ackson ametangaza nia ya kugombea Ubunge jimbo jipya la Uyole, Mbeya katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Dkt. Tulia ambaye pia ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kwa sasa ni Mbunge wa Mbeya Mjini.

Alitoa msimamo huo Ijumaa iliyopita, Mei 23, 2025, huku akisema ameamua kufanya hivyo ili kuwahudumia wananchi wa Uyole kutokana na kasi ndogo ya maendeleo iliyopo katika eneo hilo.

“Maendeleo ya Uyole yanasonga kwa taratibu sana, nimeona ni vyema nijitoe kwa moyo wote kuhakikisha wananchi wa Uyole wanapata huduma stahiki na maendeleo ya haraka...”

“Nitoe wito kwenu, watu wengi watakuja kwenu, chagueni kiongozi, chagueni mtumishi, itasaidia sana kuendelea kuyakimbiza maendeleo ya jamii,” alisema Dkt. Tulia.

Alisema hatua ya kugawanywa kwa jimbo la Mbeya Mjini na kupata jimbo jipya la Uyole, kunaleta maumivu, kwa kuwa kutokana na upendo uliopo...”

“Wengi wamekuwa wakijiuliza mbunge anaenda au anabaki, na kwamba kama ingewezekana angegombea tu yote mawili, lakini sasa kwa kuwa hilo haliwezekani ni kwamba analazimika kuwenda katika jimbo jipya...”

“Upande wowote nitakaousema hapa msiwe na wasiwasi, kwa kusema hivyo ndugu zangu wa Mbeya Mjini, na kwa kufahamu kazi tuliyofanya pamoja, na kwa kufahamu kwamba mimi bado nitakuwa mzazi wa watoto wawili, sina budi kuelekea kwa mtoto anayehitaji zaidi...”

“Na hii hakuna mtu anayeagwa leo ila kuna



kusema Tulia atagombea wapi na hakuna yeyote atakayekosa huduma yoyote aliyokuwa anaipata...”

“Wana wa Jimbo la Mbeya Mjini nimeona hapa kuna watu mioyo imeinama, lakini msiname kwa sababu bado mimi nipo,” alisisitiza.

Kwa mara ya kwanza, Dkt. Tulia ambaye amewahi kuwa mhadhiri wa sheria wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliwania ubunge wa Mbeya Mjini mwaka 2020 na baada ya kushinda alifanikiwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.


Kabla ya wakati huo, mara ya kwanza kuanza kujulikana nje ya duru za kisheria ilikuwa ni Februari mwaka 2014, wakati Rais Jakaya Kikwete alipomteua kuingia katika Bunge Maalumu la Katiba akiwakilisha Jumuiya na Taasisi za Elimu ya Juu, kisha kumteua kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipofika Septemba mwaka 2015.

Uteuzi huo ulimtambulisha Dkt. Tulia kwa jamii ya Watanzania na baada ya uchaguzi wa mwaka 2015.

Miezi miwili tu katika nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Rais John Magufuli alimteua katika nafasi 10 za wabunge anazoruhusiwa kikatiba, kisha kumuingiza kuwania nafasi ya Naibu Spika wa Bunge ambapo alishinda.



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Mbunge: Wizara ishirikiane na Takukuru

Na Hellen NGOROMERA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeshauriwa kushirikiana na Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) kubaini wanaoghushi mikataba ya ardhi.

Ushauri huo umetolewa na Mbunge wa Cha-ma Cha Mapinduzi (CCM), Jimbo la Kilombero, Morogoro, Abubakar Asenga, na kusesitiza kuwa ushirikiano huo utadhibiti matapeli wa ardhi.

Amesema ushirika huu ndiyo utaukuwa mwiba na dawa ya kukomeshwa kwa utapeli un-aofanyika kwenye sekta ya ardhi, ambapo watu wengi “wanaumizwa.”

Alikuwa akichangia mjadala wa bajeti wa wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, jijini Dodoma.

“Ni imani yangu mheshimiwa waziri kama ulivyosema utafanya ziara Mkoa wa Morogoro, kutatusaidia kutatua migogoro baina ya mipaka mfano kule Sanje, Ituli na Kidatu...”

“Mheshimiwa Rais alikuja mwezi Agosti mwaka 2024 na tukizungumza kuhusu mgogoro wa ardhi pale Ifakara mjini kata ya Mlabani mbele ya Rais na Baba Askofu alikuwepo pale,” alisema.

Mbunge huyo, alisema baada ya kupewa maelezo kuhusu mgogoro huo wa ardhi uliodumu kwa miaka mingi, rais alitoa maelekezo yali-yomfanya waziri abakie eneo hilo na kukutana na wahusika.

Asenga alisema kwa kutimiza makubaliano yaliyofikiwa siku hiyo, serikali imeshatoa kiasi cha shilingi milioni 150 kati ya shilingi milioni 400 zilizohitajika kwa ajili ya kazi za utatuzi wa mgogoro huo.

Asenga ameshauri wizara hiyo kuweka mikakati ili kukabiliana na migogoro ya ardhi kwa kutumia mifumo ya kidijiti akisema matumizi ya mfumo huo yatasaidia kutatua migogoro ya ardhi kwa urahisi na haraka.

“Migogoro ya ardhi kama alivyosema mheshimiwa waziri na mheshimiwa naibu spika ni kuwaombea Mungu viongozi wetu hawa



Mbunge wa Kilombero CCM, Abubakar Asenga

kwa sababu hata hapa Dodoma ukiangalia sasa hivi naona mmemleta kamishna mpya wa ardhi anaitwa Godfrey Mwamsojo...”

“Namuona anavyokaa pale na mimi nilikuwa na migogoro yangu, nimeenda pale unao-na kabisa mpaka mvi zake zimeanza kuwa za brown (kahawia) anasikiliza migogoro mpaka anasinzia...”

“Mgogoro unaenda mbele unarudi nyuma unazunguka unaanzia mwanzo ulipoanzia. Kwa hiyo hii maana yake narudi pale kwenye hoja yako ya msingi Mheshimiwa Waziri kwamba hii kamisheni ya ardhi mkiianzisha itatusaidia kupunguza mambo haya,” alisema Asenga na kuongeza:

“Mimi kwenye jimbo langu nilipata mpango wa hati za kimila katika mji wa Ifakara wilaya ya Kilombero. Katika vitu ambavyo vimepunguza migogoro kwa asilimia kubwa ni utoaji wa hati za kimila. Ule mpango kwa sasa hivi haupo kwa sababu sisi ni Halmashauri ya mji,” aliongeza.

Alisema ikiwa kamisheni hiyo ya ardhi ikien-da kidijiti kwa kuwa na vifaa vya kisasa kama mobile trucks (magari), itasaidia kutatua kero kwa wakati.

Makala

Vanilla iliyoahidi utajiri yawaangamiza wakulima Kagera



Na Mutayoba ARBOGAST, Bukoba

BAADHI ya wakulima wa zao la vanilla katika wilaya za Misenyi, Bukoba na Muleba, mkoani Kagera, wamelazimika kung'oa miche ya zao hilo kutokana na kukosa soko la uhakika.

Tukio hilo ni marejeo ya matukio kama hayo ambayo yametokea katika kipindi cha miaka kumi iliyipita.

Hili ni pigo kubwa kwa jamii ambazo zilikuwa zimewekeza nguvu nyingi na fedha kwenye kilimo hiki kwa matumaini ya kupata faida na kuboresha maisha yao.

Mwaka 2020 ulileta matumaini mapya kwa wakulima wa vanilla, baada ya bei ya zao hilo kupanda maradufu hadi kufikia shilingi 150,000

kwa kilo moja ya vanilla mbichi.

Kupanda huko kwa bei kulitokana na kupungua kwa uzalishaji duniani, hasa nchini Madagascar ambayo ni mzalishaji mkubwa wa zao hilo duniani, baada ya vimbunga kusababisha uharibifu mkubwa wa mashamba.

Hali hiyo ilisababisha ongezeko kubwa la uzalishaji nchini Tanzania, huku wakulima wengi wakihamasika kuanza au kuongeza uzalishaji wa vanilla.

Hata hivyo, hali imebadilika kwa kasi kubwa. Wakizungumza na Pambazuko kwa nyakati tofauti, wakulima wameeleza kwa uchungu namna wanavyowekeza nguvu kubwa katika kilimo cha zao hilo kuanzia kutunza miche, kupalilia, hadi kuchavusha kwa mikono - zoezi linalohitaji umakini na muda mrefu, lakini mwisho wanaambulia 'patupu' au kulipwa bei ya chini isiyolingana na gharama na juhudi walizotumia.

"Nimelazimika kung'oa vanilla kabisa maana haina faida tena. Kama kungekuwa na mtetezi wa zao hili, tungepiga hatua kubwa," alisema John Ruta wa kata ya Buyango.

Hata hivyo, bado kuna wakulima wachache waliobaki na matumaini. George Lwabara kutoka Kata ya Kanyigo anasema; "mimi naendelea kutunza shamba langu. Siwezi kukata tamaa, naamini siku moja bei itapanda tena kama ilivyowahi kutokea huko nyuma."

Kwa mujibu wa tovuti rasmi ya Mkoa wa Kagera, mwaka 2017 wakulima wa vanilla walilipwa jumla ya shilingi bilioni 8, jambo lililoashiria kuwa zao hili linaweza kuwa chanzo kikuu cha kipato iwapo soko litakuwa thabiti.

Lakini pamoja na jitihada hizo, hali ya bei imeporomoka kwa kiwango cha kutisha. Kilo moja ya vanilla mbichi, ambayo mwaka 2020 ilinunuliwa kwa shilingi 150,000, ilishuka hadi shilingi 30,000 mwaka 2022, na mwaka 2023 ikazidi kuporomoka hadi kufikia shilingi 3,000.

Mwaka 2024, baadhi ya wakulima walilazimika kuuza kwa zao hilo kwa shilingi 2,000 tu kwa kilo, likiwa ni anguko la bei kwa zaidi ya asilimia 98 ndani ya kipindi cha miaka mitano.

Kampuni mbili kubwa za ununuzi wa vanilla, Mayawa na NEI, zimeshindwa kununua vanilla kwa misimu miwili mfululizo.

Inaendelea Uk. 23

Vanilla iliyoaihidi...

Inatoka Uk. 22

NEI imekuwa ikinunua kwa kusuasua na kampuni nyingine iitwayo Sosaka, ambayo iliingia sokoni kwa kishindo mwaka 2024 kwa ahadi ya kununua kwa bei elekezi ya serikali ya shilingi 15,000 kwa kilo, haikutimiza ahadi hiyo - badala yake ilichukua vanilla ya wakulima bila kuwalipa.

Kwa mfano, takwimu kutoka ofisi ya Ofisa Kilimo ya Kata ya Ruzinga, Misenyi zinaonesha kuwa mwaka 2020 walizalisha tani 12.6 za vanilla, tani 10.4 mwaka 2021, tani 13.8 mwaka 2022 na tani 9.6 mwaka 2023.

Ingawa uzalishaji ulikuwa mzuri, sehemu kubwa ya vanilla haikurekodiwa rasmi mwaka 2023 kwa sababu iliharibika shambani kutokana na ukosefu wa wanunuzi.

Kata hiyo ilikuwa na wakulima 756 kati ya wakazi 1,528 kwa mujibu wa sensa ya Mwaka 2022 – huku zaidi ya nusu ya wakazi wakitegemea vanilla kama chanzo kikuu cha kipato.

Mabadiliko makubwa

Mwenendo wa bei za vanilla katika soko la kimataifa pia unaonyesha mabadiliko makubwa. Mnamo mwaka 2015, bei ya kilo moja ya vanilla kwa usafirishaji kutoka Tanzania ilikuwa dola za Marekani 14 tu.

Mwaka 2016 bei ilipanda hadi dola za marejani 18.50 na mwaka 2017 ilifikia dola za Marekani 352 kwa kilo moja.

Hii ilikuwa ni ongezeko la karibu mara 20 ndani ya mwaka mmoja, jambo lililowavuta wakulima wengi kuingia kwenye kilimo hiki. Lakini hali hiyo haikudumu.

Mwaka 2019 bei ilishuka hadi dola za Marekani 302 na mwaka 2020 ikazidi kupungua hadi dola za Marekani 196.67.

Hata hivyo, mwaka 2021 ulileta matumaini mapya tena baada ya bei kupanda na kufikia dola za Marekani 1,274 kwa kilo moja - bei ya juu zaidi kuwahi kushuhudiwa.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, mwaka 2023 bei ilitarajiwa kuwa dola za Marekani 848 kwa kilo na kufikia mwaka 2024, bei ilishuka tena hadi dola za Marekani 514 kwa kilo moja.

Kutoka kilele cha dola za Marekani 1,274

hadi dola za Marekani 514 ni anguko la bei la asilimia 60 ndani ya miaka mitatu pekee, hali inayoonesha kutokuwepo kwa uthabiti wa bei duniani kote.

Licha ya bei ya zao hilo kushuka nchini, bei ya kimataifa bado inaonekana kuwa juu, jambo linaloibua maswali kuhusu mfumo wa ununuzi na usambazaji wa vanilla nchini.

Akizungumza bungeni Mei 22, 2025, Neema Lugangira - mwakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kupitia mwavuli wa Nacongo na Mbunge wa Kagera - aliikumbusha na kuisisitiza serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuweka mikakati madhubuti ya kutafuta soko la uhakika kwa zao la vanilla.

Alikumbusha ahadi ya serikali kupitia mam-laka ya Copra (Cereal and Other Produce Authority) ya kutafuta masoko nchini Japani na China itekelezwe kwa haraka.

Kwa sasa, ni wazi kuwa changamoto ya soko imetishia maisha ya maelfu ya wakulima wa vanilla mkoani Kagera.

Bila mikakati madhubuti ya kuongeza usindikaji wa vanilla hapa nchini na kuwajengea uwezo wakulima kuhifadhi au kuchakata vanilla yao hadi ipatikane fursa ya kuuza kwa bei nzuri, zao hili litaendelea kuwa donda ndugu.



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL

Sikubaliani na kauli za wabunge hawa



Mwanaharakati
kutoka Kenya,
Martha Karua

BUNGE lina utaratibu wake ambao unaongozwa na kanuni zilizotungwa kwa ajili ya kuliongoza katika kipindi chote cha uhai wake.

Wabunge wanakuwa bungeni, wanaongozwa kanuni, iwe mavazi, kauli na hata namna ya ustaarabu vikao vinapoendelea.

Huo ndiyo utaratibu wa Bunge na mara zote unaheshimiwa na wote wanaoingia bungeni, wawe ni wabunge, watumishi wengine au wageni waalikwa wanaohudhuria kwa sababu maalum zilizoruhusiwa kwa mujibu wa kanuni.

Nimelazimika kusema hivyo kwa sababu, wiki iliyopita Watanzania walikerwa na ujio wa mwanaharakati wa Kenya ambaye pia ni mwanasheria maarufu nchini humo, Martha Karua, aliyezuiwa kuingia nchini kwa ajili ya kusikiliza kesi ya uhaini inayomkabili Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu.

Baadhi ya Watanzania walimlaani Karua na wenzake, Boniface Mwangi na Agather Atuhaile wa Uganda na walisema mengi kwa sababu hawakuona sababu za msingi zilizowasukuma wa-

naharakati hao kuja Tanzania kusikiliza shauri hilo.

Miongoni mwa waliowashutumu Karua na wenzake ni baadhi ya wabunge wa Bunge letu ambao kwa bahati mbaya walitoa kauli ambazo haziendani na hadhi ya kibunge.

Wabunge wetu walichangia hoja nyingi kuonyesha ni kwa kiasi gani hawakuridhishwa na ujio wa wanaharakati hao, ila baadhi ya kauli walizotumia kuwasilisha hoja zao, hazikuwa lugha za kibunge ambazo hupaswa kudhibitiwa na kiti, kikiwa kimekaliwa na spika, naibu spika au mwenyekiti.

Najua wabunge walikuwa na hasira ndiyo maana walichangia kwa hisia kali ili mradi tu ujumbe wao uwafike.

Pamoja na yote hayo, wabunge wetu walitakiwa kuepuka lugha kali ili kulinda heshima yao na heshima ya Bunge ambalo moja ya majukumu yake ni kutunga sheria.

Kwa mfano, kuna mbunge alisema anashangaa Jeshi la Polisi kwa “kutoshughulika na kenge wa ndani” wanaoichafua nchi, kisha akaonyesha msisitizo kwa kulitaka jeshi hilo lifanye hivyo kwa kenge wa nje.

Mbunge mwingine alisimama na kusema Martha Karua alitakiwa kurudishwa kwao akiwa na mtungi wa gesi, badala ya kurudishwa akiwa salama kama alivyofanyiwa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Binafsi sikubaliani na wale wote wanaohatarisha amani ya nchi yetu, ila ninachoshauri ni wabunge kutoa hoja bila mihemko hata kama jambo wanalozungumzia linawaumiza wao na taifa kwa ujumla.

Mimi ni miongoni mwa Watanzania wanaoipenda Tanzania na ni miongoni mwa wasiofurahishwa na lugha za uchochezi zinazoweza kuwa chanzo cha mivutano baina nchi yetu na nchi jirani zikiwamo Kenya na Uganda.

Kwa hiyo, nasema sikubaliani na kauli za wabunge hao kwa sababu mbunge aliyetumia neno kenge, angeweza kutumia neno jingine la kistaarabu, lakini likimaanisha jambo lilelile na aliyetumia neno mtungi wa gesi, angeweza kutumia neno mbadala pia lisilo la kuudhi.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Deodatus Mwanyika

Kamati 'yaishukia' Wizara ya Kilimo

Na Mwandishi WETU

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, imejia juu Wizara ya Kilimo, ikisema bajeti yake haikidhi mahitaji halisi ya sekta hiyo kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014).

Maazimio hayo kwa ujumla wake yanazitaka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya bajeti ya taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo.

Hayo yameelezwa wiki iliyopita na mwenyekiti wa kamati hiyo, Deodatus Mwanyika (Njombe – CCM), wakati akiwasilisha bungeni utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Kamati hiyo pia ilitoa maoni na ushauri kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/26 ya shilingi trilioni 1.243.

Pamoja na mambo mengine, kamati imeishauri serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kwamba fedha hizo zitolewe kwa wakati ili kuwezesha kufikia malengo na mikakati iliyokusudiwa.

“Kamati inaishauri serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutenga bajeti na kuajiri maafisa ugani wa kutosha, ili kusogeza huduma kwa

wakulima wengi zaidi na kuleta tija katika kilimo kama ilivyokusudiwa,” alisema Mwanyika.

Awali, akiwasilisha bajeti hiyo, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitaja mafanikio yaliyopatikana katika sekta hiyo kwa kipindi cha miaka minne iliyopita.

Alisema mikakati ya kimuundo kuanzia upanuzi wa umwagiliaji na mifumo ya ushirika, kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje na kuongeza mauzo ya bidhaa za kilimo nje ya nchi yamechangia mafanikio hayo.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya sita ilirithi changamoto kadhaa ikiwemo ufinyu wa bajeti, uhaba wa mikopo, ukosefu wa fedha maalumu za kuendeleza kilimo, pamoja na ushiriki mdogo wa vijana na wanawake kutokana na ukosefu wa mtaji na changamoto ya umiliki wa ardhi.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, bajeti ya wizara hiyo imeongezeka kwa asilimia 324.5 kutoka shilingi bilioni 294 mwaka wa fedha 2021/22 hadi shilingi trilioni 1.248 mwaka 2024/25.

“Ukuaji wa sekta umeimarika kutoka asilimia 2.6 mwaka 2021 hadi asilimia 4.2 mwaka 2023 na makadirio ni kukua kwa asilimia tano mwaka 2025 na asilimia 10 ifikapo 2030.

Inaendelea Uk. 26

Habari**Kamati ‘yaishukia’...****Inatoka Uk. 25**

“Thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi iliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.2 mwaka 2019/20 hadi dola za Marekani bilioni 3.54 mwaka 2023/24 ikiwa ni ongezeko la asilimia 195,” alisema Bashe.

Kwa upande mwingine, alisema uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kwa asilimia 33 kutoka tani milioni 17.14 mwaka 2021/22 hadi tani milioni 22.8 mwaka 2023/24 na kufikia asilimia 128 ya kujitosheleza kwa chakula nchini karibu na lengo la asilimia 130 kitaifa.

Kuhusu hifadhi ya chakula, Bashe alisema uwezo wa hifadhi ya chakula kitaifa umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 209, kutoka tani 251,000 mwaka 2020/21 hadi tani 776,000 mwaka 2024/25.

Alisema pia kuwa idadi ya miradi ya umwagiliaji imeongezeka kutoka 13 mwaka 2020/21 hadi 780 mwaka 2024/25, yenye thamani ya shilingi trilioni 1.34 ikihudumia hekta 543,366.

Bashe alisema ukamilishaji wa miradi hiyo utaongeza eneo la umwagiliaji hadi hekta 1.27 milioni na kwamba miradi ya ushirika imeongezeka kutoka 19 hadi 912.

Hata hivyo, Bashe alikiri kuwa hadi mwaka wa fedha 2020/21 sekta ya kilimo ilikuwa imebaki kama sekta inayokwenda kwa kudra za Mwenyezi Mungu na jitihada binafsi za wakulima.

Alisema hatua hiyo ilitokana na uwekezaji hafifu na usio wa uhakika wa serikali na shughuli za kilimo kutotambulika katika mfumo rasmi.

Hali hiyo iliamsha Wizara ikatengeneza na kutangaza mpango mkubwa wa kutoa huduma za zana za kilimo kwa wakulima nchini kwa bei nafuu kupitia ruzuku kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026.

“Wizara itaanzisha vituo 1,000 vya utoaji huduma za zana, kununua matrekta 10,000, power tiller 10,000 pamoja na zana nyingine za msingi za kilimo ikiwemo mashine za kuvunia na kukaushia mazao.

“Serikali itaanzisha huduma za zana za kilimo ambapo wakulima watalipia kwa bei ya ruzuku, ili kuondoa kikwazo cha gharama kwa wakulima

wadogo,” alisema Bashe.

Alisema serikali imeongeza viwanda vina-vyomilikiwa na vyama vya ushirika kutoka 267 mwaka 2021/2022 hadi 331 mwaka 2024/2025 vikijihusisha na uchambuaaji wa pamba; ukoboaji wa mpunga, kahawa na mahindi.

Vyama vingine vinajihusisha na usindikaji wa maziwa; ukamuaji wa mafuta ya pamba, alizeti, karanga na ufuta; na ubanguaji wa korosho.

“Akiba katika vyama vya akiba na mikopo (Saccos) imeongezeka kutoka shilingi bilioni 576 hadi shilingi bilioni 966.9, wakati mikopo iliyotolewa kwa wanachama imeongezeka kutoka shilingi bilioni 798 hadi shilingi trilioni 1.1 na ripoti za ukaguzi safi zimeongezeka kutoka 339 hadi 631,” alisema Bashe.

Ajibu hoja za wabunge

Akijibu hoja za wabunge kuhusu wawekezaji, Bashe alisisitiza kuwa ili nchi iendeleo ni lazima uchumi ushikiliwe na wananchi wenyewe.

“Tukifanya makosa ya kuhakikisha uchumi wote unashikiliwa na wageni hautamsaidia mtanzania wa kawaida,” alisisitiza.

Kuhusu Chama Kikuu cha Ushirika wa Pamba, Bashe aliwaambia wabunge kuwa chama hicho kimekuwa kikipata bajeti ya shilingi bilioni moja, lakini fedha hizo zimekuwa zikitumika kwa matumizi ya kawaida.

“Hizi fedha wanazitumia kwa matumizi ya kawaida tu, hawawekezi popote, zinaishia kwenye vikao, mikutano, posho. Tunafanya nini? Kweli tuiache Shirecu namna hiyo? Itakuwa ni kosa kubwa sana. Kwa hiyo, wakulima wa pamba tutahakikisha tunawasaidia waongeze tija na vipato vyao,” alisema.

Hata hivyo, alisema haitakuwa rahisi kupata tija katika kilimo cha pamba endapo viongozi kutoka kanda ya pamba hawatakubali kubadilika na kuzingatia misingi ya kisayansi katika uzalishaji wa zao hilo.

Alisema miongoni mwa changamoto kuu katika uzalishaji wa pamba ni kukataa misingi ya kisayansi.

“Licha ya kuelekezwa kuwa wakulima wasi-changanye mazao mengine katika mashamba ya pamba, bado wengi wanaendelea kufanya hivyo, jambo linalopunguza tija na ubora wa zao hilo,” alisema Bashe.



‘Magwajima’ na haja ya kuokoa Bunge



Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima

KAULI ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa Mei 30, 2025 katika Mkutano Mkuu Maalum wa CCM jijini Dodoma, imeacha gumzo, mijadala, na tafakuri nzito kuhusu mwenendo wa viongozi wa chama hicho tawala.

Katika hotuba hiyo, Rais Samia alisema; “Lazima tuwe makini sana kuchuja wagombea wa nafasi mbalimbali. Tusirudie tena kule kuingiza watu wasiofaa. Wengine hadi tunasema huyu ni Magwajima! Unampa ubunge anakurukia.”

Kauli hiyo imefasiriwa na wachambuzi wa siasa kama kumlenga moja kwa moja Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, ambaye wiki moja kabla aliikosoa serikali kuhusu matukio ya utekaji.

Rais Samia, akiwa Mwenyekiti wa CCM, ameonyesha kutoridhishwa na tabia ya baadhi ya viongozi waliopewa heshima kubwa kupitia chama akiwemo Gwajima, lakini wanaitumia nafasi hiyo kuichafua serikali yao hadharani

badala ya kutumia vikao halali vya chama kueleza hoja zao.

Kulingana na baadhi ya wachambuzi, kauli ya Rais Samia ni sura ya wazi kuwepo kwa mvutano wa ndani ya chama, ambapo baadhi ya viongozi wanaanza kujisafisha kisiasa kwa kujenga umaarufu wa upinzani wa ndani, jambo ambalo linaweza kuhatarisha mshikamano wa CCM kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025.

Kauli za hadharani kama za Askofu Gwajima zinaweza kuzua mashaka kwa wananchi kuhusu mshikamano wa chama na uwezo wake wa kusimamia viongozi wake walioko serikalini.

Rais Samia alitumia jina “Magwajima” kwa kejeli, kuonesha kutoridhishwa na uteuzi wa watu wasiokuwa na uadilifu wa kisiasa na nidhamu ya chama.

Alitaka kuonya dhidi ya tabia ya kuwapitisha watu wanaojali umaarufu wao binafsi kuliko maslahi ya wananchi na chama.

Ni ujumbe wa wazi kwa sekretarieti ya chama, kamati kuu, na wajumbe, kwamba mchujo wa wagombea kwa uchaguzi mkuu wa 2025 lazima uwe makini kupita kawaida na zaidi ya kuwa mazoea.

Kwamba chama kisiendeleo kujifunga bao kwa mikono kwa kuwaweka watu wasiostahili kwenye nafasi nyeti kama ubunge au udiwani.

Hoja yangu ni kwamba, kauli ya Rais Samia juu ya “Magwajima” siyo tu kejeli ya kisiasa, bali ni mwito wa maadili, nidhamu, na ukomavu wa siasa ndani ya CCM.

Ni fursa ya chama hicho kusimama upya, kujihoji, na kuchuja kwa uangalifu wale wote wanaotaka kuliongoza taifa kupitia dhamana ya chama.

Ikiwa kauli hiyo itachukuliwa kwa uzito, inaweza kuwa mwanzo wa kusafisha siasa zetu; lakini ikipuuzwa, wanaweza kuwepo wengi wanaoweza kuibuka na kwenda kinyume cha taratibu za chama hicho tawala kujisimamia vyema zaidi.

Mwandishi anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Riwaya

Viaticum-36

Sakramenti ya Mwisho



Kwa wasomaji wapya: Mambo ndiyo yanazidi kupamba moto na kushika kasi. Jeshi la Polisi linakomaa na uchunguzi wa kifo, je, nini kitafuata? Endelea kusoma riwaya hii tamu.

Na Godwin Chilewa, Houston, MAREKANI

WAKATI wataalam wa uchunguzi wa eneo la tukio wakiendelea na kazi yao kundi la wapelelezi lilikuwa likizunguka kuhoji majirani na watu wanaofanya biashara katika maeneo ya karibu.

Wote hao walieleza kushitushwa kwao kwa mauaji ya Masenya. Licha ya kuwa marehemu alikuwa mtu mwenye roho nzuri na moyo wa kusaidia wengine, lakini pia kifo chake kilikuwa cha kutisha sana.

Police Constable (PC) Awadhi alikuwa mmojawapo wa wapelelezi waliokuwa wakihoji majirani.

Wote aliowahoji aliwauliza maswali yaliyolenga kumtambua muuaji, na au sababu za kuua-

wa kwa kijana huyo mpore.

Mmoja wa watu aliozungumza nao alikuwa jirani wa Masenya aitwae mzee Mahamood.

“Mzee wangu hebu niambie, Masenya alikuwa na ugomvi na mtu?” PC Awadhi alimuuliza kwa heshima.

“Hapana, alikuwa mtu mwema na mpole sana, watu wengi walimpenda kwa sababu alikuwa mtu wa msaada sana. Kila msiba ulipotokea hapa tulikwenda kumuona ili atusaidie kushughulikia mwili na kuhifadhi.”

“Unafahamu kama alikuwa akidaiwa na mtu yeyote au tabia ya dhuruma?”

“Mh, hilo sina hakika nalo sana, lakini kwa kadri nijuavyo hakuwa mtu wa kukopakopa hata kidogo.”

“Alikuwa akitumia madawa ya kulevya kama kokeni, heroini, bange au aina nyingine yoyote?”

“Hilo sina hakika. Wakazi wa hapa tulikuwa tunahisi huenda alikuwa akivuta bange, lakini hatukuwahi kumuona akivuta.”

“Kwanini mnadhani alikuwa akivuta bange?”

“Kwa sababu ya kazi yake. Mwanangu, kupasua maiti si kazi rahisi, mtu wa kawaida huwezi kuifanya, lazima uvute bange. Lakini kama nilivyosema sikuwahi kumuona wala kumsikia. Hata pombe alikuwa akinywa kidogo tu, hakuwa mlevi,” mzee huyo alieleza kwa ufasaha.

“Vipi kuhusu uzinzi? Alikuwa na tabia ya kutembea na wake za watu?” PC Awadhi alihoji.

“Hapana, hilo siwezi kumsingizia. Yeye alipendelea zaidi kuchukua makahaba, mwenyewe alikuwa akiwaita madada poa. Siku moja aliwahi kuniambia huwa anawaona wanawake wa Butimba kama dada zake tu, maana wanamuo-gopa kwa sababu ya kazi yake.”

“Kama hakuwa na mke alikuwa akijipikia mwenyewe au alikuwa akila kwa mama ntilie? PC Awadhi aliuliza kwa mshangao kidogo.

“Sina uhakika, ila mara nyingine nilikuwa nikimuona akila chipsi pale Cheru Bar.”

“Alikuwa akijishughulisha na biashara yoyote ile? Iwe ya harali au ya haramu?”

“Sidhani kama alikuwa na biashara maana hilo lingejulikana tu. Kila alipotoka kazini alienda kupoteza muda pale Cheru Bar,” alieleza Mahamood.

Inaendelea Uk. 29

Viaticum-36

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

PC Awadhi hakuona jipya. Alishayasikia maelezo kama hayo zaidi ya mara ishirini. Kila Jirani aliyezungumza naye alimsifia Masenya kwa wema na ukarimu wake; lakini kila aliyemuuliza kama alimuona mtu yeyote akiingia au kutoka nyumbani kwa Masenya kati ya saa kumi na mbili na nusu jioni na saa mbili usiku, hakuna aliyekuwa na maelezo, kila mtu alidai hakuona chochote.

Hatimaye akaamua kwenda Cheru Bar. Hapo aliwakuta wapelelezi watatu wakizungumza na watu mbalimbali.

Bar yenyewe ilikuwa imejaa mno, na asilimia kubwa ya wateja walikuwa wameshaanza kulewa. Kwa vile wenzake walikuwa ndani ya jengo kuu yeye akaamua kukaa nje.

Akachagua meza iliyokuwa tupu, akakaa hapo. Mhudumu alipomuona akamfuata haraka.

“Habari za jioni kaka,” mhudumu huyo alimsalimu.

“Salama kabisa, hujambo?”

“Sijambo, nikusaidie kinywaji gani?”

“Nipatie CocaCola baridi,” alimwambia huku akimpa noti ya shilingi elfu tano. Mhudumu akaipokea, akaondoka kwenda kufuata kinywaji.

Baada ya muda mfupi, akarudi akiwa na chupa ya soda na glasi. Akaweka vitu hivyo meza ni, akafungua soda, akaimimina kwenye glasi, akamkaribisha.

“Ahsante dada. Sasa naomba uketi kitini mara moja, nina maswali machache nataka kukuuliza,” PC Awadhi alimwambia mhudumu huyo huku akimuonesha kitambulisho chake.

Binti wa watu hakubisha. Akaweka chini sinia aliloshika, akavuta kiti akakaa.

“Naitwa Konstebo Awadhi kutoka Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai - Kituo Kikuu cha Polisi, tuko hapa kufuatilia tukio la mauaji lililotokea jioni hii, naamini umepata habari.”

“Ndiyo” mhudumu huyo alijibu kwa wasi-

wasi.”

“Usiwe na hofu dada, huu ni uchunguzi wa kawaida unaofanyika kila tukio la aina hii linapotokea. Vilevile wewe si mtu pekee unayehojiwa na polisi, watu wengi wanaoishi na kufanya kazi au biashara katika eneo hili wame-shahojiwa, na wengine watahojiwa baadae.

Lengo letu ni kupata taarifa zitakazolisaidia Jeshi la Polisi kumpata muuaji kabla hajaua mtu mwingine,” PC Awadhi aliongea kwa sauti ya upole kumtoa wasiwasi.

“Nimeelewa kaka.”

“Unaitwa nani?”

“Naitwa Aisha Abdallah” Alijibu kwa sauti ya uchangamfu kidogo, PC Awadhi akatoa kitabu chake cha kumbukumbu akaandika.

Alipomaliza akamuuliza tarehe yake ya kuzaliwa, kabila, dini, anuani ya makazi, namba ya simu, jina la mwenyekiti wake wa serikali ya mtaa, mahali anapofanya kazi, jina la bosi wake, na namba ya simu ya bosi wake. Haya yote akayaandika kwenye kitabu chake cha kumbukumbu.

“Kama nilivyokwambia mimi na wenzangu tuko hapa kufanya uchunguzi wa kifo cha jirani yenu, Masenya aliyeuawa kikatili saa chache yaliyopita. Kwa hiyo naomba uwe huru kuniambia lolote linaloweza kunisaidia” PC Awadhi alisisitiza.

“Sawa nimeelewa,” Aisha alijibu.

“Ulikuwa ukimfahamu Masenya?”

“Ndiyo, nilikuwa nikimfahamu.”

“Ulimfahamia wapi?”

“Hapa hapa, alikuwa akija mara kwa mara kula chakula, na mara nyingine kupumzika tu”

“Ulikuwa na mazoea naye?”

“Kila mtu wa hapa alikuwa amemzoea, alikuwa kijana mcheshi na mwenye roho nzuri sana”

“Mara ya mwisho ulimuona lini?”

“Leo jioni kwenye saa kumi na mbili jioni. Alikuwa kununua soda na bia” Aisha alijibu huku sauti yake ikionesha kutetemeka kidogo.

“Wewe ndiye ulimuhudumia?”

“Hapana, alihudumiwa na mhudumu mwingine anaitwa Rose, ila alipokuwa akiondo-ka alinisemesha.

Itaendelea wiki ijayo...

Barua za wasomaji**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba;
+255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

Chadema kiache ubabe**Mhariri,**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimekuwa kikitunishiana misuli na Msajili wa Vyama vya Siasa, hadi kufikia hatua mlezi huyo wa vyama vya siasa nchini kukifutia ruzuku chama hicho.

Awali, msajili alikiandikia chama hicho barua kuwa hatambui sekretarieti na wajumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, hivyo kiitishe baraza kuu ili kupata viongozi hao.

Lakini, Chadema kupitia Kamati Kuu yao kiliazimia kutokujibu barua kwa kile walichodai ofisi ya msajili haina mamlaka ya kufanya hivyo.

Matokeo yake msajili amesimamisha ruzuku ya chama hicho.

Ni vyema sasa Chadema kupitia kikao chake cha Kamati Kuu kinakachofanyika kesho Juni 3, 2025, wasirudie makosa.

Miriam Joackim**Barabara ya 12, Tanga.****Elimu ya kuwa mbunge angalau iwe shahada****Mhariri,**

NI jambo lililo dhahiri kwamba mabadiliko makubwa yanahitajika kuhusu namna ya kuwapata wabunge wa Tanzania.

Kwa sasa kigezo kikubwa cha mtu kuchaguliwa kuwa mbunge, ni kujua kusoma na kuandika.

Tunawaona wabunge wengi namna wana-vyochangia hoja bungeni wanaonekana kuwa na uwezo mdogo na wengine ni kama hawajitam-bui.

Mfano; inawezekanaje mbunge kuwaita wana nchi ni kenge? Huo ni mfano mmoja tu, lakini kuna mlolongo mrefu ya michango ya wabunge ambayo ukisikiliza unaona maajabu.

Ni vyema kigezo cha elimu kianzie shahada na kusiwe na wabunge wa viti maalum.

Anney Frank**+44 2036197893, Uingereza.****Terminal 2 JNIA imeachwa yatima!****Mhariri,**

JUZI nilibahatika kusafiri kwa ndege kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Safari yangu ilinilazimu nitumie jengo la terminal 2 ambalo kabla ya ujenzi wa terminal 3 ndilo lilikuwa jengo kuu kwa usafiri kutokea uwanjani hapo.

Tangu terminal 3 izinduliwe, sijatumia terminal 2 na niliyoyaona wiki iliyopita yamenisikisha sana.

Ni kwamba terminal hiyo imeachwa kama mtoto yatima.

Maduka na huduma zote ndani ya terminal, ukiacha maduka yaliyoko kwa nje, hayapo tena – yamehamishiwa terminal 3. Hakuna mgahawa

wowote unaofanya kazi.

Yaani zaidi ya huduma za maliwato, hakuna huduma nyingine ya kijamii ambayo inapatikana ndani ya jengo la terminal 2!

Hii inasikitisha sana. Mtu ukishikwa na kiu au njaa, ukishaingia kwenye jengo hilo, basi inahitaji huruma ya maofisa ili upate chakula au kinywaji.

Ukiwa umesahau kubadili fedha (kama unaenda nje ya nchi), basi sahau kupata huduma hiyo ndani ya terminal 2.

Naziomba mamlaka ziangalie jinsi ya kurejesha huduma, hasa za migahawa na maduka ya kubadilishia fedha, katika jengo hilo ili kuwanusuru abiria ambao wanateseka sana hivi sasa.

Joseph Mkatamali,**Ubungo – Dar es Salaam.**

Kariakoo kukata bima kupitia pango



Mkuu wa Mkoa wa
Dar es Salaam, Albert
Chalamila

Na Hellen NGOROMERA

UKOSEFU wa bima za ajali katika maeneo mbalimbali, umeamsha Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam kuamua kujumuisha malipo ya bima kupitia kodi ya pango kwa wafanyabiashara wa Soko la Kimataifa la Kariakoo.

Hatua hiyo itasaidia kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara ana bima na hivyo kunapotokea janga lolote kila mmoja atakuwa na uhakika wa kulipwa bima.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema hayo wiki iliyopita jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya ujenzi wa soko hilo unaokaribia kukamilika.

“Wakati soko linaungua, hakukuwa na bima, hivyo sasa bima itaingizwa kwenye kila kodi ya pango inayolipwa, ni muhimu sana kuzingatia bima ambayo lazima soko kabla halijaanza kufanyika, tuhakikishe kwamba limekatiwa bima kutoka kwenye insurance (bima) maalumu ili in case (iwapo) kwa baadaye kukiwa na hitilafu bima ibebe mzigo huo,” alisema Chalamila.

Alisema serikali ilitoa shilingi bilioni 28.3 kulijenga na kulikarabati soko hilo na kwamba hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 98.

Kuhusu ulinzi na usalama kwa ujumla, alisema mifumo ya kamera itafungwa sokoni hapo ili kusaaidia kufuatua na kubaini mienendo ya watu wazuri na wabaya wanaokusudia kufanya majaribio ya aina yoyote katika eneo hilo.

Alisema wafanyabiashara watakaofanya biashara katika soko hilo watarudi baada ya

kukubaliana na masharti yatakayowekwa.

Alitaja moja ya masharti hayo kuwa ni kuhakikiwa na kusajiliwa katika mfumo na kwamba serikali ndiyo itabeba jukumu la kupanga bei ya pango.

“Kwa sasa tume-avoid (epuka) madalali ambao wengi walikuwa wakichukua zaidi ya eneo moja na kisha kuwapangisha wengine...”

“Yapo baadhi ya maduka ambayo yataratibiwa upya kwa kutangazwa katika mfumo wa tausi ili wafanyabiashara wenye nguvu waombe,” alisema Chalamila.

Aliwakata wafanyabiashara wadogo waliofunga barabara kwa kuweka meza ambazo zinazuia watu na magari kuingia kwa urahisi sokoni hapo kwa ajili ya kuingiza bidhaa mbalimbali ndani ya soko hilo, waondoke katika kipindi cha wiki mbili.

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Masoko Kariakoo, Ashraf Abdulkarim, alisema kuna maeneo 1,520 ya biashara na kwamba wafanyabiashara waliojisajili kwenye mfumo wa Tausi kwa kujaza fomu ni 1,159.

Alisema wafanyabiashara hao wamegawanika katika makundi matatu ambayo ni wafanyabiashara wa vizimba, viuatilifu na vifungashio ambao wamepangiwa kufanya biashara katika ghorofa ya tatu hadi ya tano na kundi la pili ni la wafanyabiashara watakaofanya biashara mbalimbali waliojisajili kwenye mfumo wa Tausi. Alisema wafanyabiashara wa kundi la tatu watatangaziwa utaratibu leo (Juni 2), ili wajisajili. Wafanyabiashara hao wametengea eneo la wazi.

Makala

Waandishi wa habari sasa kutambuliwa rasmi

Na Hellen NGOROMERA

SEKTA ya habari na utangazaji inahesabika kama mhimili wa nne wa dola ambao si rasmi, pembeni ya Serikali, Bunge, na Mahakama.

Hii ni kutokana na umuhimu wa kazi zake ambazo zinaiunganisha mhimili hiyo rasmi na jamii. Ni kupitia kwa vyombo vya habari mhimili hiyo inaweza kuwasiliana na jamii kwa haraka na urahisi, jambo ambalo lianwezesha kusukuma mbele jitihada za ku-liendeleza taifa.

Lakini kwa muda mrefu sekta ya habari imevam-iwa na watu ambao wamekuwa wakifanya kazi zake na kukiuka maadili ya taaluma ya habari, ikiwemo kutangaza vitu vyenye maudhui yanayokiuka maadili.

Kutokana na hali hiyo, serikali iliamua kuunda

Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB) kupitia Sheria ya Huduma za Habari, ikiwa na lengo la kuimarisha weledi, uwajibikaji na heshima ya taaluma ya uandishi wa habari nchini.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Tido Mhando, anasema katika mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni kuwa bodi hiyo imeanzishwa ili kuvisimamia vyema vyombo vya habari kwa lengo la kulinda maadili na weledi wa taaluma hiyo.

“Kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya vyombo vya habari kumekuwa pia na ongezeko kubwa la idadi ya waandishi wa habari wanaofanya kazi katika vyombo vya habari, jambo ambalo linahitaji usimamizi wa kitaaluma ili kuhakikisha waandishi wa habari wanafanya kazi kwa kufuata maadili ya taaluma yao.

“Hivyo, serikali ilitambua umuhimu wa kuwa na sheria inayosimamia sekta ya habari ili kukuza weledi, na kwa mantiki hiyo, ilianzisha Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari ambayo ilizinduliwa rasmi Machi 3, 2025 na waziri wa Habari, Sanaa, Michezo na Utamaduni, Palamagamba Kabudi,” anasema Mhando.

Anaeleza kwamba bodi hiyo ina majukumu kadhaa yaliyoainishwa kwa mujibu wa sheria ikiwemo kuwathibitisha waandishi wa habari wenye sifa na kuwapatia vitambulisho; kusimamia uzingatiaji wa maadili ya taaluma ya waandishi wa habari; kuzingatia viwango vya kitaaluma na kukuza maadili mazuri

ya taaluma.

Kwa mujibu wa taratibu zilizotangazwa na JAB, maombi ya ithibati ya waandishi wa habari wanaotaka kupatiwa vitambulisho (press cards) yatafanyika mtandaoni kupitia mfumo unaoitwa TAI-Habari.

Hatua hiyo inalenga kuboresha huduma, kuimarisha usimamizi wa taaluma ya uandishi wa habari na kurahisisha upatikanaji wa vitambulisho kwa waandishi waliothibitishwa.

Mhando anabainisha kuwa tofauti na miaka ya nyuma, kuanzia mwaka huu maombi ya vitambulisho vya waandishi watawasilishwa na waandishi wenyewe.

“Hapo zamani chombo cha habari kilikuwa kinaweza kuleta orodha ya waandishi wake na kuwaomba vitambulisho. Lakini hivi sasa kila mwandishi anayehitaji kitambulisho atalazimika yeye mwenyewe kujaza fomu kwenye mtandao,” anafanua. Fomu hiyo inapatikana kupitia kiunganishi <https://www.taihabari.jab.go.tz> ambako muombaji atakutana na maelekezo ya nini anapasa kufanya.

Akishajaza taarifa za awali zinazotakiwa, mwombaji atapokea msimbo kupitia ujumbe mfupi kwenye simu yake au barua pepe ili kuendelea na hatua za kujaza wasifu, kufanya maombi, kupata ankara ya malipo kulipia na kuwasilisha maombi ya kupata kitambulisho. Mwenyekiti huyo anataja mahitaji muhimu wakati wa kuomba ithibati na kitambulisho kuwa ni pamoja na mwandishi kuwa na namba ya simu na barua pepe vinavyofanya kazi, picha ndogo iliyoskaniwa, vyeti vya elimu vilivyoskaniwa kwa mfumo wa PDF na kuthibitishwa na mamlaka husika (kwa chuo kikuu vithibitishwe na TCU na kama ni vyuo vya kati vithibitishwe na NACTVET).

Pia mwombaji atatakiwa kuwa na barua ya utambulisho kutoka katika taasisi anayoifanyia kazi au anakopeleka kazi zake ikiwa ni mwandishi wa kujitegemea, nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) pamoja na ada ya ithibati ambayo ni shilingi 50,000.

“Ada hiyo ni ya muda wa uhai wa kitambulisho ambao ni miaka miwili,” anasema Mhando.

Anasema kwa waandishi wa habari wa kigeni pia watafuata utaratibu huu kuwasilisha nyaraka kama mfumo utakavyowaelekeza na ada kwa waandishi hao wa kigeni ni dola za kimarekan 500.

Inaendelea Uk. 33

Waandishi wa habari...

Inatoka Uk. 32

“Mahitaji hayo ni muhimu ili kukamilisha mchakato wa maombi kwa mafanikio. Baada ya kuwasilisha maombi, mwombaji atapokea ujumbe wa SMS kuonyesha hatua ya maombi yake kama yanashughulikiwa, yamekubaliwa, yamerudishwa kwa marekebisho, au yamekataliwa. “Ikiwa maombi yatakuwa yamekubaliwa, Bodi itamjulisha mwombaji mahali na muda wa kuchukua kitambulisho chake,” anafafanua.

Mhando anataja majukumu mengine ya Bodi hiyo kuwa ni kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusiana na masuala ya habari, kuweka viwango vya taaluma na mafunzo kwa waandishi wa habari; kuanzisha ushirikiano na taasisi nyingine za aina hiyo ndani na nje ya nchi; kuandaa mafunzo kwa waandishi wa habari; kutunza orodha ya waandishi wa habari waliothibitishwa; kusimamia hesabu za fedha, mali na madeni ya Bodi; na kutekeleza kazi zingine ambazo Waziri anaweza kuelekeza.

“Kuthibitishwa au kupewa Ithibati na Bodi kunakuza hadhi na heshima ya taaluma ya uandishi wa habari kama ilivyo kwa taaluma nyingine kama sheria na udaktari. Uandishi wa habari unapaswa kutambuliwa rasmi kama taaluma yenye hadhi na umuhimu mkubwa katika jamii,” anasema Mhando.

Anasema kupitia ithibati, waandishi wa habari wanapata utambulisho rasmi unaowawezesha kufanya kazi zao kwa heshima na uadilifu.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, sekta ya habari na utangazaji hapa nchini na duniani kote imepitia mabadiliko makubwa yanayotokana na maendeleo ya teknolojia ambayo yamewezesha upatikanaji wa taarifa na kuongeza idadi ya vyombo vya habari.

“Mabadiliko haya yameimarisha demokrasia na utawala bora, yamehimiza uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza, na yamefanya upatikanaji wa habari kuwa rahisi na wa haraka zaidi,” anasema Mhando.

Anasema kutokana na maendeleo hayo ya teknolojia kumekuwa na njia za kisasa za kukusanya, kuchakata, na kusambaza habari; kuibuka kwa taasisi zinazolinda na kutetea maslahi ya vyombo vya habari na waandishi wa habari; kuongezeka kwa taasisi zinazotoa elimu ya uandishi wa habari na mawasiliano na kuanzishwa kwa vitengo vya mawasiliano serikalini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za serikali.

Pia teknolojia imewezesha kuanzishwa kwa televisheni na redio za mtandaoni; mabadiliko kutoka mfumo wa utangazaji wa analogia kwenda wa dijitali; na kuongezeka kwa matumizi ya mitandao ya kijamii katika usambazaji wa habari,” amesema Mhando.

Anaeleza kuanzishwa kwa bodi hiyo ni hatua muhimu katika mchakato wa kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari kwa kuhakikisha kuwa wanahabari wanazingatia viwango vya juu vya weledi, maadili na uwajibikaji. Lakini kwa upande mwingine, Mhando anabainisha kuwa kumekuwa na taarifa za kuwepo kwa baadhi ya watu wanaojaribu kuwasilisha vyeti vya kughushi au nyaraka zisizo halali kwa lengo la kujipatia usajili na vitambulisho.

Mhando ameonya kwamba waandishi wa habari watakaobainika kuwasilisha vyeti au nyaraka za kughushi watachukuliwa hatua kali bila kujali hatua waliokuwa wamefikia katika mchakato wa usajili.

“Hatua hizi zitajumuisha kufutiwa mara moja usajili wao, kuwasilishwa katika vyombo vya sheria kwa ajili ya kuchukuliwa hatua stahiki, pamoja na kupigwa marufuku kujihusisha na shughuli za uandishi wa habari au majukwaa mengine ya kitaaluma.

“Ni muhimu kukumbuka kuwa Mfumo wa TAI-Habari umeanzishwa kwa nia njema ya kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari kwa misingi ya uwajibikaji, weledi na heshima lengo ni kuhakikisha kuwa kila mwandishi aliyesajiliwa ni mtu mwenye sifa stahiki, mafunzo sahihi, na anayezingatia maadili ya kazi hii muhimu,” anasema Mhando.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Joyce Shebe, ametoa rai kwa waandishi wa habari kuipenda na kuilinda tasnia hiyo kwa wivu mkubwa kwa kutumia kalamu zao vizuri kwa manufaa ya taifa.

“Tuipende na tuilinde kwa wivu mkubwa ili mwisho wa siku tuitumie kalamu zetu kwa ajili ya kuisaidia nchi kupiga hatua kimaendeleo,” amesema Shebe. Amewataka waandishi wa habari kutopokea taarifa ya kujisajili katika mfumo huo mpya kama kitu kibaya bali kuuchangamkia kwa ari kubwa.

“Ni ukweli usiopingika kwamba fani yetu imevamiwa na watu wengi wanafanya uandishi wa habari. Kila mwenye simu akipiga picha na kurusha mtandaoni anaonekana kama ni mwandishi wa habari.

“Kuna watu ambao hawana ABCD za uandishi wa habari na utangazaji ni vyema wasio na taaluma wakasome,” amesema Joyce.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles



Bongo kama Met Gala

MET Gala ni tamasha la mitindo ya mavazi ambalo huwakutashisha watu maarufu duniani lililoanzishwa mwaka 1948, linalofanyika kila mwaka likilenga kukusanya fedha kwa ajili ya Makumbusho ya Costume ya Metropolitan huko Manhattan New York, Marekani.

Katika siku hii, watu maarufu duniani wakiwemo wanamuziki, waigizaji, wanamichezo na nyanja nyingine, hukusanyika kwa kila mmoja kuibuka na ubunifu wa hali ya juu ili kuweza kutikisa watazamaji.

Ndivyo unaweza kusema katika siku tano zilizopita, ambapo msanii wa nyimbo za Bongo Fleva, Juma Jux na mkewe, Priscilla Ojo, alifanya sherehe yake ya nne ya harusi Jumatano iliyopita katika ukumbi wa Superdome Masaki, jijini Dar es Salaam.

Sherehe hii ilitanguliwa na nyingine zilizofanyika nchi Nigeria baada ya ndoa iliyofungwa Februari 7, 2025.

Hapa nchini imehudhuriwa na mastaa wengi katoka nyanja tofauti ambao walilipuka kisawasawa kwa mavazi yenye ubunifu mkubwa.

Wengi waliohudhuria sherehe hiyo walijitahidi kwenda na rangi za harusi hiyo ambazo zilikuwa rangi mbili tu, nyeusi pamoja na ile ya dhahabu.

Mastaa waliovutia kwa kupendeza ni Jux na mkewe hasa vazi la pili la mwanamke, Diamond Platinumz, Zuchu hasa vazi la pili lilikuwa simpo, Ommy Dimpoz, Dulluvan, Paula, Marioo, Sishkiki, wapambe wa maharusi wa kike na kiume, Lavish gauni zote.

Ms. Love, Auntie Ezekiel, Glory, Monalisa Sseiwa, Niffer, Tahiya John na Lulu Diva karibu nguo zote nne zilikuwa nzuri ingawa ya pili ilikuwa kawaida.

Wapo waliovaa ikawa kawaida kama Nandy katika vazi la kwanza ingawa la pili lilikuwa bora likingeshwa na nakshi ya kofia, Jacky Wolper lakini kuna waliopania wakapitiliza kama Irene Uwoya vazi la kwanza, Zuchu vazi la kwanza.

Wapo pia ambao waliharibu kwa rangi tofauti kama Dayna Nyange na Rushaina (hili jina lipitie uone) na aliyeharibu zaidi kama mwanamuziki Phina.

Ondoa mafuta usoni

USO wenye mafuta huwa una kawaida ya kutoa mafuta unapotembea au unapopakaa poda au make up.


Zipo njia za kufanya ili kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na matumizi ya mdalasini, ndimu na asali.

*Chukua mdalasini wa unga kijiko kimoja, weka ndimu kijiko kimoja na asali kijiko kimoja kisha changanya kwenye bakuli,

*Pakaa usoni kisha kaa kwa muda wa nusu saa kisha nawa na maji ya uvuguvugu.

*Mchanganyiko huu unavuta usoni na kunyonya mafuta kwa uhakika. Fanya hivyo mara kwa mara unapopata nafasi.

Kwa maoni na ushauri: piga simu 0656531217

Na Anti
MSHAURI

Uhusiano



Usikubali msongo wa mawazo ukutese

MSONGO wa mawazo au stress kwa Kimombo, ni hali ambayo humpata mtu kutokana na kuwaza kupita kiasi.

Hali hiyo huanzia pale mlengwa anapokubali kuendeshwa na mawazo yanayomtawala akilini.

Wakati mwingine hali hiyo humjia mlengwa kwa kuwaza mambo ambayo hayana mashiko; wengine - hasa wanawake, huwaza kuhusu namna wanavyosengenya na marafiki na mengine yanayofanana na hayo.

Msongo wa mawazo pia humjia mtu kutokana na changamoto za kifamilia kwa kushindwa kutimiza malengo aliyoyapanga, changamoto za kazini za kijamii na nyingine.

Ukipata hali hiyo hutakiwi kuhangaika kwa kuwaza kupitiliza bali kutafuta njia sahihi za kutatua changamoto hizo.

Wakati mwingine uchovu wa majukumu mbalimbali unaweza kumfanya mlengwa kushindwa kujimudu kukabiliana nayo hivyo kujikuta akipata msongo wa mawazo.

Kuna njia mbalimbali za kukabiliana nayo

kama vile kujichanganya na watu kwa kutenga muda wa kukaa kwenye maeneo tofauti na kuzungumza na ndugu, jamaa na marafiki kwani kushikilia mawazo pekee yakuandame kwa kuyalundika akilini kunaweza kusababisha matatizo.

Kama ni mpenzi wa kuogelea unaweza kutumia muda wako kutembelea katika maeneo ya fukwe za bahari na kubadilishana mawazo na marafiki na watu wengine.

Mambo hayo yanaweza kufanywa pia na watu ambao hawana mawazo ya kupitiliza kwa kutenga muda wao na kuchangamana na wengine ili kuweka akili sawa.

Wakati mwingine 'stress' zipo lakini kinachojalisha ni nini unafanya baada ya kuwa nazo kwani hicho ndio kitaamua uendelee kuwa nazo au urudi katika hali ya kawaida. Usikubali zikutese, jipambanie kuzikataa.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.



PSG yaona mwezi Ulaya



Na Mwandishi WETU

KLABU ya Ufaransa, Paris Saint-Germain, imeshinda kombe ya Klabu Bingwa Ulaya kwa mara ya kwanza kwa staili ya aina yake kwa kuiangushia Inter Milan kipigo kitakatifu.

Katika mechi ya fainali iliyochezwa huko Munich nchini Ujerumani, PSG iliicharaza Inter kwa magoli 5-0 na kuweka rekodi ya kuwa mechi ya fainali ya ushindi wa magoli mengi.

Imeipiku fainali ya mwaka 1994 ambapo mahasimu wa Inter, AC Milan waliichabanga Barcelona kwa magoli 4-0 katika fainali.

Hii ni mara ya kwanza kwa PSG kunyakua kombe hilo kubwa barani Ulaya baada ya juhudi zake za miaka lukuki.

Kama ilivyotarajiwa, mechi hiyo ilichezwa kwenye mazingira tulivu uwanja lakini nje ya uwanja kulitawaliwa na vurugu za hapa na pale na kusababisha vifo vya watu wawili.

Ndani ya uwanja ilikuwa ni fainali ya upande

mmoja kwani PSG waliutawala mchezo huo katika mipindi vyote.

PSG inakuwa timu ya pili ya Ufaransa kushinda kombe hilo baada ya Marseille kufanya hivyo mwaka 1993.

Ilikuwa ni siku nzuri kwa mshambuliaji kindi wa PSG na Ufaransa, Desire Doue, mwenye umri wa miaka 19, ambaye aliingia kambani mara mbili baada ya kutengeneza goli la kwanza lililofungwa na beki wa pembeni Achraf Hakimi.

Magoli mengine yalifungwa na Khvicha Kvaratskhelia na Senny Mayulu aliyeingia kipindi cha pili.

“Sina maneno ya kulielezea tukio hili. Hii ni ndoto yangu kubwa. Tumeandika historia,” alisema Doue baada ya mechi hiyo.

Kiungo fundi Mreno ambaye alikuwa mmoja wa walioisaidia PSG kushinda, Vitinha, naye alisema: “Hii inamaanisha kila kitu. Ni ndoto yangu, ni ndoto yetu. Ni furaha sana. Matokeo haya si miuji-za. Nina furaha sana kuwa tumeshinda namna hii, sasa acha tukasherehekee.”

Timu hiyo inayomilikiwa na matajiri kutoka Qatar imepata ushindi huo miaka mitano baada ya kupoteza katika fainali dhidi ya Bayern Munich. Hiyo ndiyo ilikuwa mara yao ya kwanza kufika fainali na tangu hapo hawajafika tena hatua hiyo.

Vurugu

Hata hivyo, sherehe za ushindi huo zilileta dosari kubwa baada ya watu wawili kufariki akiwamo kijana mwenye umri wa miaka 17 aliyechemwa kisu katika mji wa Dax kusini mwa Ufaransa.

Askari polisi mmoja alipoteza fahamu katika vurugu hizo huku watu kadhaa wakikamatwa.